# HOTUBA YA WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA MHESHIMIWA CHARLES N. KEENJA (MB.) KUHUSU MAKADIRIO YA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA 2003/2004

## I. UTANGULIZI

**1.** Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Kilimo na Mifugo inayohusu Wizara ya Kilimo na Chakula na baada ya kuzingatia taarifa hiyo, naomba kutoa hoja, kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupitisha makadirio ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo ya Wizara ya Kilimo na Chakula kwa mwaka wa fedha wa 2003/2004.

**2.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2002/2003 ambao unamalizika leo, viongozi wetu Wakuu wa Kitaifa, walikipa kilimo umuhimu wa juu katika shughuli zao za kila siku. Wakuu hao wametoa maelekezo mbalimbali muhimu juu ya hatua za kuchukuliwa ili kuongeza wingi na ubora wa mazao yanayozalishwa humu nchini kwa lengo la kujitosheleza kwa chakula, kuondoa umaskini na kuongeza mauzo ya mazao nje ya nchi. Walipotembelea mikoa, walitenga muda kukagua kilimo na kutoa maelekezo ya hatua za kuchukuliwa ili kukifanya bora zaidi. Aidha, wametoa maelekezo ya kisera yaliyolenga kuweka misingi ya kukuza uzalishaji na mapato yatokanayo na kilimo, ikiwa ni pamoja na kuongeza sehemu ya mapato ya Serikali inayowekezwa katika kilimo kama ilivyofanyika mwaka wa 2002/2003 na itakavyofanyika mwaka huu. Nawashukuru sana kwa kazi zao nzuri.

**3.** Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2002/2003 **nchi nzima** ilikumbwa na ukame uliotokana na mvua kukatika mwezi wa Januari, 2003 hadi Aprili, 2003. Hali hiyo iliathiri vibaya mazao yaliyokuwa mashambani na kuashiria Taifa kuathiriwa na upungufu mkubwa wa chakula na hata njaa. Tarehe 31 Machi, 2003, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, alilihutubia Taifa, chini ya utaratibu wake wa kuzungumza na wananchi kila mwezi. Katika hotuba hiyo, Rais alifafanua hali mbaya ya chakula iliyoelekea kujitokeza na akaagiza hatua za kuchukuliwa na kila ngazi ya jamii kukabiliana na hali hiyo. Mungu alisikia kilio chetu na hali sasa siyo mbaya kama ambavyo ilielekea kuwa. Aidha, wananchi wengi waliitikia wito wa Rais wetu na wakapanda mazao aliyoelekeza kwa wingi. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais na pia nawashukuru sana wananchi wote walioitikia wito wa Rais wa kulima mazao ya kujikinga na njaa. Nitajadili hali ya chakula kikamilifu zaidi chini ya aya ya 13 hadi 16.

**4.** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimwa Eliachim J. Simpasa, Mbunge wa Mbozi Magharibi, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Kilimo na Mifugo na Waheshimiwa Wabunge wote walioteuliwa kuwa wajumbe wa Kamati hiyo. Katika kipindi kifupi tangu Kamati hii iteuliwe, imekutana na Wizara kupata maelezo kuhusu muundo na majukumu ya Wizara, Bodi za Mazao, mashirika na asasi zilizoko chini ya Wizara. Mwezi wa Mei, 2003, Kamati ilitembelea Taasisi ya Utafiti wa Mazao ya Kilimo, Mikocheni na mashamba makubwa ya miwa na viwanda vya kusindika sukari vya Kilombero na Mtibwa na ilipata fursa ya kukutana na wakulima wadogo wa miwa katika maeneo hayo na kutoa mchango mkubwa wa mawazo na maelekezo ya kuboresha uzalishaji wa zao hilo.

**5.** Kamati ilipokea na kuchambua kwa makini Taarifa ya Utekelezaji ya Wizara ya Kilimo na Chakula ya Mwaka wa 2002/2003 na Makadirio ya Matumizi ya Mwaka wa 2003/2004. Kamati ilitoa maelekezo kuhusu mambo ambayo yanapaswa kuzingatiwa ili kuweka msisitizo katika kuondoa vikwazo na matatizo yanayokifanya kilimo kisikue kwa kasi ya kuridhisha. Maelekezo na maoni ya Kamati yamezingatiwa katika mapendekezo niyowasilisha mbele ya Bunge hili Tukufu na yataendelea kuzingatiwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

**6.** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuwapongeza kwa dhati Wabunge wote walioshinda katika chaguzi ndogo za tarehe 18 Mei, 2003. Wabunge hao ni: Mhe. Abu Towagale Kiwanga (Mb.), CCM, Jimbo la Kilombero; Mhe. Nazir Mustafa Karamagi (Mb.), CCM, Jimbo la Bukoba Vijijini; Mhe. Edward Nziriye Ndeka (Mb.), CCM, Jimbo la Kigoma Kusini; Mhe. Sumri Abdallah Salum Mohamed (Mb.), CCM, Jimbo la Mpanda Magharibi; Mhe. Karim Said Othman (Mb.), CUF, Jimbo la Chambani; Mhe. Masoud Abdalla Salim (Mb.), CUF, Jimbo la Mtambile; Mhe. Mohamed Juma Khatibu (Mb.), CUF, Jimbo la Chonga; Mhe. Ali Said Salim (Mb.), CUF, Jimbo la Ziwani; Mhe. Shoka Khamis Juma (Mb.), CUF, Jimbo la Micheweni; Mhe. Salim Omar Alli (Mb.), CUF, Jimbo la Tumbe; Mhe. Mchande Salim Mchande (Mb.), CUF, Jimbo la Konde; Mhe. Mohamed Ali Said (Mb), CUF, Jimbo la Wingwi, Mhe. Khamis Ally Saleh (Mb.), CUF, Jimbo la Mgogoni; Mhe. Khalifa Suleiman Khalifa (Mb.), CUF, Jimbo la Gando; Mhe. Khalifa Mohamed Issa (Mb.), CUF, Jimbo la Mtambwe; Mhe. Bakari Shamis Faki (Mb.), CUF, Jimbo la Ole, Mhe. Mwadini Abass Jecha (Mb.), CUF, Jimbo la Utaani; Mhe. Ali Said Juma (Mb.), CUF, Jimbo la Kojani na Mhe. Omar Juma Omar (Mb.), CUF, Jimbo la Pandani.

**7.** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumshukuru Naibu Waziri wa Kilimo na Chakula, Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala, Mbunge wa Namtumbo; Katibu Mkuu, Ndugu Wilfred Ngirwa; Wakuu wa Idara na Taasisi na Asasi zilizoko chini ya Wizara, watumishi wote na wadau wa Sekta ya Kilimo kwa ushirikiano na ushauri wao katika mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2003. Watendaji hawa wameshiriki kikamilifu katika kutekeleza Mpango wa Kilimo wa Mwaka wa 2002/2003. Aidha, wamechangia katika kuandaa taarifa mbalimbali, ikiwemo Taarifa ya Utekelezaji ya Mwaka wa 2002/2003 na Makisio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka wa 2003/2004, ambayo ninaiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu.

**8.** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Fredrick Tluway Sumaye (Mb.); Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba (Mb.) na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Mheshimiwa Dk. Abdallah Omari Kigoda (Mb.) kwa hotuba zao nzuri. Hotuba zao zimechambua na kufafanua masuala muhimu ya kiuchumi na ya kijamii, ikiwa ni pamoja na hali ya kilimo na chakula nchini na hatua zinazochukuliwa kuongeza uwekezaji ili kukifanya kilimo kikue kwa haraka zaidi. Nawapongeza Wabunge waliochangia na kujadili hotuba hizo kwa michango yao mizuri na ushauri wao ambao tutauzingatia katika kuongeza ukuaji wa sekta ya kilimo.

**9.** Mheshimiwa Spika, maelezo aliyotoa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika hotuba yake kwa Taifa tarehe 31 Machi, 2003 na uchambuzi, maelekezo na ushauri uliotolewa na Waziri Mkuu, Waziri wa Fedha, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Mipango na Ubinafsishaji na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za mikoa na Serikali za Mitaa, yasomwe pamoja na, na kuchukuliwa kuwa ni sehemu ya hotuba hii.

## II. HALI YA KILIMO NCHINI

**10.** Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka minne iliyopita, kilimo kilianza kuonyesha dalili za kuongeza kasi ya kukua. Mwaka wa 1999, kilimo kilikua kwa asilimia 4.1, mwaka wa 2000 asilimia 3.4, mwaka wa 2001 asilimia 5.5. Katika mwaka wa 2002, kilimo kilikua kwa asilimia 5, na hivyo kutokufikiwa kwa lengo la asilimia 6.0 kutokana na kushuka kwa bei za mazao makuu ya biashara hususan, kahawa, pamba na chai. Ukuaji huu mdogo hauwezeshi kufikiwa kwa malengo ya kufufua uchumi na kuondoa umaskini kwa kasi ya kuridhisha. Utafiti uliofanywa na Wizara ya Kilimo na Chakula na Benki ya Dunia mwaka wa 2000, unaonyesha kwamba ili kilimo kiweze kuchangia ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini kwa kasi ya kuridhisha, inabidi kikue kwa zaidi ya asilimia 10 kwa mwaka.

**11.** Kasi ndogo ya ukuaji wa sekta ya Kilimo, inasababishwa kwa kiasi kikubwa na hali mbaya ya hewa, hususan ukame, uwekezaji mdogo katika sekta ya Kilimo, milipuko ya magonjwa, wadudu na wanyama waharibifu wa mimea na mazao na matumizi madogo ya teknolojia. Matatizo mengine ni pamoja na kukosekana kwa masoko ya uhakika na yenye bei nzuri kwa mazao yetu makuu ya biashara na kushuka sana kwa bei za mazao hayo. Kilimo kinakabiliwa pia na janga la UKIMWI linaloathiri sana nguvukazi. Changamoto iliyoko mbele yetu ni kuondoa matatizo haya ili kuruhusu kilimo kukua na kuondoa umaskini miongoni mwetu kwa kasi kubwa zaidi kwa kuzingatia malengo ya kuondoa umaskini.

### Hali ya Chakula kwa Mwaka wa 2002/2003

**12.** Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa chakula kwa mwaka wa 2002/2003 ilikuwa nzuri. Taifa lilijitosheleza kwa asilimia 102. Hali hii ilitokana na uzalishaji wa mazao ya chakula wa jumla ya tani milioni 8.5, zikiwemo tani milioni 4.1 za nafaka na tani milioni 4.4 za mazao yasiyo nafaka katika msimu wa 2001/2002, ikilinganishwa na miaka miwili iliyotangulia ambapo Taifa lilijitosheleza kwa asilimia 92 mwaka wa 2000/2001, na asilimia 94 katika mwaka wa 2001/2002. Aidha, mwanzoni mwa msimu wa 2002/2003, kulikuwa na alibaki ya tani 379,000 za msimu wa 2001/2002. Hali hiyo nzuri ya chakula iliwezesha nchi yetu kuuza chakula nje ya nchi na kutoa msaada wa tani 3,000 za chakula kwa Serikali ya Zimbabwe. Kati ya mwezi wa Julai, 2002 na Mei, 2003, tuliuza nje ya nchi tani 151,291 za mahindi, tani 38,233 za maharage, tani 3,354 za mchele, tani 29,387 za ngano, tani 80 za mtama na uwele, tani 477 za ndizi na tani 72 za muhogo. Wakati huo huo tuliagiza kutoka nje ya nchi tani 256,293 za ngano na tani 24,110 za mchele.

**13.** Pamoja na hali ya chakula kuwa nzuri Kitaifa, katika mwaka wa 2002/2003, kulikuwepo na maeneo machache katika baadhi ya mikoa ambayo yalikuwa na upungufu wa chakula. Maeneo hayo yalikuwa katika mikoa ya **Arusha,** wilaya za Monduli na Ngorongoro; **Manyara**, wilaya ya Simanjiro na **Kilimanjaro** wilaya za Same, Mwanga na Moshi Vijijini. Upungufu wa chakula katika maeneo hayo ulitokana na mvua kunyesha kwa viwango vidogo na kwa mtawanyiko mbaya. Tathmini ya kubaini watu walioathiriwa na upungufu wa chakula iliyofanywa mwezi wa Novemba, 2002, ilibaini kuwa kulikuwa na watu 176,000 waliohitaji msaada wa chakula kati ya miezi ya Januari na Machi, 2003. Serikali ilitenga jumla ya tani 7,200 za chakula kutoka Hifadhi ya Chakula ya Taifa (SGR) kuwa hudumia watu walioathirika na njaa. Aidha, Shirika la Mpango wa Chakula Duniani,

kwa kutumia utaratibu wa chakula kwa kazi, lilitoa jumla ya tani 445 za chakula katika wilaya za Manyoni, Dodoma, Nzega, Kwimba, Iramba na Misungwi.

### Matarajio ya Chakula kwa Mwaka wa 2003/2004

**14.** Mheshimiwa Spika, ufuatiliaji wa hali ya mvua na ya mazao mashambani uliofanywa na Wizara umeonyesha kwamba maeneo makubwa ya nchi yatakuwa na upungufu wa chakula katika mwaka wa 2003/2004. Hali hiyo inatokana na mabadiliko ya hali ya hewa katika msimu wa 2002/2003 yasiyotarajiwa na ambayo yalisababisha upungufu mkubwa na kutokutabirika kwa mvua katika maeneo yote ya nchi. Mvua zilikatika katikati ya mwezi wa Januari hadi wiki ya tatu ya mwezi wa Machi, 2003 na kuathiri vibaya ukuaji wa mazao yaliyokuwa mashambani. Katika baadhi ya maeneo, hali ni mbaya zaidi kwa kuwa wananchi walilima mazao yasiyostahimili ukame, hali inayoashiria udhaifu katika usimamizi wa kilimo.

**15.** Tathmini ya awali ya uzalishaji wa mazao ya chakula nchini kwa msimu wa 2002/2003 inaonyesha kuwa uzalishaji wa mazao ya chakula utafikia tani milioni 7.55, zikiwemo tani milioni 3.84 za mazao ya nafaka na tani milioni 3.71 za mazao yasiyo nafaka. Makisio ya mahitaji ya chakula katika mwaka wa 2003/2004 yanatarajiwa kuwa tani milioni 8.37. Kwa hiyo, Taifa linatarajia kujitosheleza kwa chakula kwa asilimia 90 tu (Kiambatanisho Na. 1). Aidha, katika mwaka wa 2003/2004 inatazamiwa kwamba kutakuwapo albaki ya tani 450,000 kutoka msimu wa 2002/2003. Hadi tarehe 16 mwezi wa Juni, 2003 Hifadhi ya Chakula ya Taifa ilikuwa na tani 51,971 za chakula, maghala ya wafanyabiashara yalikuwa na tani 114,899 na kiasi cha tani 333,740 zilikuwa mikononi mwa wananchi. Albaki hii ya jumla ya tani 500,610 inafanya pengo la chakula lipungue kutoka tani 817,500 hadi tani 316,890.

**16.** Mheshimiwa Spika, pamoja na hali ya uzalishaji wa chakula kitaifa kutokuwa ya kuridhisha, mikoa ya Iringa, Rukwa, Mbeya, Ruvuma, Kigoma, Kagera na Mtwara itajitosheleza kwa chakula na kuwa na ziada. Aidha, kutokana na mvua zilizoendelea kunyesha kati ya mwezi wa Machi hadi mwanzoni mwa mwezi wa Juni, 2003, mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Mwanza, Mara na Tabora inatarajiwa kujitosheleza kwa chakula. Mikoa iliyosalia itakuwa na upungufu wa chakula na itajitosheleza kwa viwango vinavyotofautiana kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini.

| *Jedwali Na. 1: Maeneo yaliyoathiriwa zaidi na Upungufu wa Chakula mwaka wa 2003/2004* | | | |
|---|---|---|---|
| **MKOA** | **Kujitoshe - leza %** | **WILAYA** | |
| | | **Wilaya Zilizoathirika** | **Wilaya Zinazojitosheleza / Zenye Ziada** |
| Manyara | 69 | Simanjiro (tarafa zote) Hanang (tarafa zote), Kiteto (tarafa za Kibaya na Kijingu) na Babati (tarafa za Mbugwe na Babati) | Mbulu |
| Arusha | 69 | Monduli | Arumeru, Arusha na Ngorongoro |
| Dodoma | 72 | Dodoma Vijijini, Kongwa na Kondoa | Mpwapwa |
| Pwani | 73 | Bagamoyo (Tarafa ya Msoga) na Kisarawe (tarafa za Mzenga, Chole na Sungwi) | Kibaha, Mkuranga, Mafia na Rufiji |
| Lindi | 76 | Ruangwa (tarafa za Ruangwa, Mandawa na Mnacho) na Kilwa | Liwale, Lindi na Nachingwea |
| Singida | 78 | Singida Vijijini, Manyoni na Iramba | |
| Shinyanga | 84 | Meatu na Kishapu | Bukombe, Kahama, Maswa, Bariadi na Shinyanga Vijijini |
| Morogoro | 84 | Mvomero (Tarafa\ya Mlali), Morogoro Vijijini (Tarafa ya Ngerengere) | Ulanga, Kilosa na Kilombero |
| Mwanza | 91 | | Sengerema, Geita, Ukerewe, Kwimba, Magu na Misungwi |
| Mara | 97 | | Musoma, Tarime, Serengeti na Bunda |
| Tabora | 97 | | Tabora, Igunga, Uyui, Urambo na Nzega |
| Tanga | 100 | | Tanga, Lushoto, Muheza, Kilindi, Pangani, Handeni na Korogwe |
| Kilimanjaro | 100 | | Moshi Vijijini, Hai, Rombo, Same na Mwanga |
| Ruvuma | 107 | | Songea/Namtumbo, Tunduru na Mbinga |
| Mbeya | 116 | | Mbeya, Rungwe, Mbozi, Ileje, Kyela na Mbarali |
| Mtwara | 118 | Masasi | Mtwara na Tandahimba, |
| Kagera | 120 | | Bukoba, Muleba, Biharamulo, Ngara na Karagwe |
| Kigoma | 124 | | Kigoma, Kasulu na Kibondo |
| Rukwa | 127 | | Sumbawanga, Nkasi na Mpanda |
| Iringa | 128 | Iringa Vijijini (Tarafa ya Isimani) | Njombe, Mufindi, Makete na Ludewa |
| *Chanzo:* | *Wizara ya Kilimo na Chakula* | | |

**17.** Kati ya miezi ya Januari na Aprili, 2003 bei za mazao makuu ya chakula zilipanda na kulikuwapo upungufu wa baadhi ya vyakula kwenye masoko. Kwa mfano, bei za zao la mahindi zilipanda kwa wastani wa asilimia 5 kutoka shilingi 13,471 hadi shilingi 14,193 kwa gunia la kilo 100, na bei ya mchele ilipanda kwa asilimia 38 kutoka shilingi 30,508 hadi shilingi 42,172 kwa gunia la kilo 100. Hata hivyo, kwa zao la maharage ambalo hulimwa kwa nyakati tofauti katika maeneo mbali mbali ya nchi, bei ya wastani ilishuka kwa asilimia tatu, kutoka shilingi 39,066 mwezi wa Januari hadi shilingi 37,838 mwezi wa Aprili, 2003 kwa gunia la kilo 100. Kupanda huko kwa bei hutokea kila mwaka katika kipindi hiki. Kuanzia mwezi wa Mei, 2003, bei za vyakula kwenye masoko zimeshuka na kurudia hali ya kawaida kutokana na wakulima kuvuna mazao ya msimu wa 2002/2003. Kwa jumla, hali ya chakula kwenye maeneo mengi ya nchi bado ni nzuri.

## Hatua Zilizochukuliwa na Serikali Kukabiliana na Tatizo la Ukame

**18.** Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kusema, tarehe 31 Machi, 2003, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Benjamin William Mkapa, alilihutubia Taifa juu ya **hali ya chakula nchini na mwelekeo wake katika msimu wa 2003/2004.** Katika hotuba hiyo, Rais alichambua hali ya mvua na chakula na mwelekeo wa hali ya chakula katika msimu wa 2003/2004 na akaagiza hatua zifuatazo zichukuliwe na ngazi mbalimbali za Serikali na wananchi:-

(1) Kuhakikisha maeneo yote yaliyokwisha kuandaliwa kwa kilimo cha umwagiliaji maji, yakiwemo mashamba ya NAFCO, yanalimwa kwa ukamilifu;

(2) Kuweka usimamizi wa wataalam wa umwagiliaji na kilimo kwenye mashamba yote makubwa yenye miundombinu ya umwagiliaji ambao watahakikisha kwamba mahitaji yote muhimu yanapatikana kwa wakati na kwamba waliogawiwa mashamba hayo wanayalima kikamilifu;

(3) Kuhimiza wananchi kuvuna maji ya mvua na kuyatumia kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji maji;

(4) Viongozi wa Serikali na Chama cha Mapinduzi ngazi ya mikoa na Wilaya kuhamasisha wananchi, kufuatilia kwa makini na kisayansi mwenendo wa hali ya hewa, hali ya kilimo na hali ya mazao mashambani;

(5) Kila mkoa kuandaa na kutekeleza mpango maalum wa kujihami na hali mbaya ya chakula inayoweza kujitokeza;

(6) Kuanzisha Kamati za Njaa katika kila ngazi, kuanzia mkoani, wilayani hadi kijijini. Kamati hizo zilitakiwa kutathmini hali halisi, na kubuni mikakati ya kukabiliana na upungufu wa chakula kwa kujitegemea katika kila ngazi;

(7) Kuhamasisha wafanyabiashara ndani ya nchi ili waagize chakula kutoka nje ya nchi;

(8) Kila mkulima kujiwekea akiba hadi atakapokuwa na uhakika wa mavuno ya msimu wa 2003/2004;

(9) Wananchi wa mikoa yenye chakula cha kununua na ambao hawana akiba ya chakula cha kutosheleza mahitaji ya familia hadi mavuno yajayo kujinunulia chakula cha akiba;

(10) Wananchi kulima mazao yanayostahimili ukame na yanayokomaa haraka katika msimu mmoja;

(11) Mikoa yote yenye maeneo yanayofaa kwa kilimo cha kiangazi kulimwa na kupandwa mazao ya chakula; na

(12) Wafugaji kuuza mifugo yao wakati ambapo iko katika hali nzuri na kutumia fedha watakazopata kujinunulia chakula.

**19.** Kutokana na taarifa kutoka kwenye Wilaya na timu za wataalam na viongozi zilizotumwa mikoani kutathmini hali ya mvua na mazao mashambani, maelekezo ya Rais yalipokelewa vizuri na wananchi na katika maeneo mengi ya nchi yalitekelezwa kwa juhudi ya kuridhisha sana. Nawapongeza sana wananchi wote waliotekeleza maelekezo ya Rais na Viongozi wao waliowahimiza na kuwasimamia.

**20.** Katika mwaka wa 2002/2003, Serikali ilitoa fedha za nyongeza, shilingi milioni 105 kwa ajili ya kukarabati miundombinu ya umwagiliaji maji mashambani katika skimu 14 zenye jumla ya hekta 4,517. Aidha, shilingi milioni 27.776 zilitengwa kwa ajili ya kufufua matrekta saba yaliyoko kwenye Kituo cha Utafiti na Chuo cha Kilimo cha Ilonga, Kilosa. Aidha, Serikali ilitenga shilingi milioni 173.22 kwa ajili ya ununuzi wa mbegu za mazao yanayokomaa katika muda mfupi. Wizara imewaagiza wahandisi wa Kanda za Umwagiliaji na mameneja wote wa mashamba kusimamia kilimo katika mashamba hayo. Utekelezaji wa maagizo hayo unaendelea vizuri.

**21.** Mheshimiwa Spika, katika maeneo yote yaliyokuwa na upungufu wa mvua **ambako wananchi** wamelima **muhogo kwa wingi, hakuna upungufu wa chakula.** Kule ambako uhimizaji wa kilimo cha muhogo ulikuwa hafifu au wananchi walikaidi kulima zao hilo la chakula, kuna kilio cha upungufu wa chakula na kuitaka Serikali ipeleke chakula kwenye maeneo hayo. Kama ilivyo aibu kwa nchi kuomba chakula kutoka nchi nyingine hasa inapokuwa hakuna maafa yaliyotokea, ndivyo pia inavyopasa kijiji, kata au wilaya kuona aibu ya kuomba chakula wakati ulikuwapo uwezekano wa kuzalisha chakula katika eneo linalohusika. Kuanzia sasa, **viongozi watakaozembea katika kuwahimiza wananchi**

**walime mazao yanayostawi katika mazingira yao, watawajibishwa kwa kosa la kuhatarisha maisha ya wananchi wa maeneo yao.**

## Hatua za Kuchukuliwa Kukabiliana na Upungufu wa Chakula

**22.** Taarifa zinaonyesha kwamba hakuna mkoa ambao wilaya zake zote zimeathiriwa na ukame kwa viwango vinavyolingana. Aidha, ni mikoa minne tu ambayo imeathiriwa kwa kiasi kikubwa na ukame. Mikoa kumi na saba itajitosheleza kwa chakula na mingine itakuwa na viwango tofauti vya ziada. Inaagizwa kwamba:

(a) Kusiwepo vizuizi vya aina yoyote vya kusafirishwa kwa chakula kutoka sehemu moja ya nchi kwenda sehemu nyingine ya nchi.

(b) Wafanyabiashara wahimizwe kununua chakula kutoka kwenye maeneo yenye chakula cha ziada na kukiuza kwenye maeneo yenye upungufu wa chakula.

(c) Hifadhi ya Chakula ya Taifa itawauzia wafanyabiashara watakaoteuliwa mahindi na kusimamiwa na viongozi wa mikoa na wilaya ili wayasambaze kwenye maeneo yenye upungufu.

(d) Aidha, SGR itanunua mahindi kutoka kwenye mikoa yenye ziada na kukipeleka kwenye kanda zenye upungufu ili kikasambazwe kwenye maeneo yenye upungufu wa chakula kwa utaratibu ulioelezwa hapo juu.

(e) Pale Idara ya Maafa ya Ofisi ya Waziri Mkuu itakaporidhika kwamba jamii fulani inahitaji msaada maalum wa chakula, itaweka utaratibu wa kuiuzia jamii hiyo chakula kwa masharti nafuu au kuwapa chakula kwa kazi.

**23.** Mheshimiwa Spika, tunatarajia kwamba katika mwaka wa 2003/2004 tutajitosheleza kwa chakula kwa asilimia 90. Wizara ya Kilimo na Chakula imekwishazungumza na wafanyabiashara na kuwaomba waagize tani 350,000 za mahindi, tani 223,000 za ngano, na tani 167,500 za mchele. Kiasi hicho kitatosha kuziba pengo linalotarajiwa. Mwezi huu, Kampuni ya Export Trading ilipakua tani 750 za mahindi kwenye bandari ya Mtwara kwa ajili ya mkoa wa Lindi, Wilaya za Ruangwa na Kilwa.

**24.** Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza mazungumzo na baadhi ya wahisani kwa lengo la kuwajulisha hali ya chakula ilivyo nchini na kuona kama wataweza kutusaidia kukabiliana na upungufu uliopo. Aidha, katika Bajeti ya 2003/2004, Hifadhi ya Chakula ya Taifa imetengewa fedha za kununua chakula kutoka humu nchini na Serikali imetenga fungu la fedha la dharura ambalo litasaidia kuagiza chakula kutoka nje ya nchi, kama itabidi. Ni dhahiri kwamba Serikali ya Awamu ya Tatu ya Chama Cha Mapinduzi imechukua hatua madhubuti kukabili hali ya upungufu wa chakula katika maeneo mbalimbali ya nchi.

**25.** Mheshimiwa Spika, maelekezo aliyotoa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, katika hotuba yake ya tarehe 31 Machi, 2003 na uchambuzi, maelekezo, na ushauri uliotolewa na Waziri Mkuu Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye, Waziri wa Fedha, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Mipango na Ubinafsishaji na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, katika hotuba zao zilizotangulia, yasomwe pamoja na, na kuchukuliwa kuwa ni sehemu ya hotuba hii.

## Hali ya Chakula Nchi za Jirani

**26.** Mheshimiwa Spika, taarifa ya Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) ya mwezi wa Juni, 2003 kuhusu uzalishaji wa chakula, inaonyesha kuwa katika mwaka wa 2003/2004, nchi za kusini mwa Afrika za Zambia, Malawi, Msumbiji,

Swaziland, Namibia na Angola zitakuwa na hali ya chakula ya kuridhisha. Nchi ya Zimbabwe itakuwa na upungufu wa chakula kutokana na hali mbaya ya ukame na kupungua kwa maeneo yaliyopandwa mazao ya chakula.

Mheshimiwa Spika, taarifa za FAO zinaonyesha kuwa katika mwaka wa 2003/2004 nchi za Kenya na Uganda zitakuwa na hali ya chakula ya wastani. Migogoro ya kisiasa na vita katika nchi za Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo itafanya hali ya chakula katika nchi hizo kuendela kuwa mbaya.

## Uzalishaji wa Mazao ya Biashara

**27.** Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2002/2003, uzalishaji wa mazao makuu ya biashara, hususan korosho, kahawa, pamba, sukari, chai, tumbaku na mkonge uliongezeka ikilinganishwa na uzalishaji wa mwaka wa 2001/2002, kama inavyoonyeshwa kwenye Jedwali Na. 2. Uzalishaji wa zao la korosho ulikua kwa asilimia 33.6, kahawa asilimia 45, pamba asilimia 27.5, sukari asilimia 16.0 na chai asilimia 13.3. Ukuaji wa mazao ya tumbaku na mkonge ulikuwa mdogo ambapo tumbaku ilikua kwa asilimia 3.1 na mkonge asilimia 0.4. Ukuaji mdogo wa zao la tumbaku unatokana na bei ndogo wanayolipwa wakulima iliyosababisha baadhi yao kutolima tumbaku. Zao la mkonge lilikumbwa na matatizo ya wawekezaji kushindwa kuendeleza mashamba waliyonunua na hivyo kuathiri uzalishaji. Uzalishaji wa pareto ulishuka kwa asilimia 14.3 kutokana na tatizo la ukosefu wa soko.

*Jedwali Na. 2: Uzalishaji wa Mazao ya Biashara (2000/2001-2002/2*

| Zao | Uzalishaji (Tani) | | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2000/2001 | 2001/2002 | 2002/2003 | Asilimia ya Ongezeko 2001/2002 |
| Korosho | 122,283.00 | 67,369.00 | 90,000.00 | 33.60 |
| Kahawa | 58,134.00 | 36,175.00 | 52,439.00 | 44.95 |
| Pamba | 123,558.00 | 149,091.00 | 188,690.00 | 27.50 |
| Sukari | 135,534.00 | 163,994.00 | 190,120.00 | 16.00 |
| Chai | 26,385.50 | 24,732.32 | 28,028.13 | 13.30 |
| Tumbaku | 28,000.00 | 31,700.00 | 32,693.62* | 3.10 |
| Mkonge | 20,500.00 | 23,540.00 | 23,641.00 | 0.40 |
| Pareto | 1,850.00 | 3,500.00 | 3,000.00 | -14.30 |

*Chanzo: Bodi za Mazao, 2003*

** = Matarajio*

## Mazao yasiyo Asili

**28.** Mheshimiwa Spika, kutokana na bei za mazao makuu ya biashara kuendelea kuwa za chini katika soko la dunia, Serikali inaendelea kuandaa mbegu na vipando na kuwahamasisha wakulima kuzalisha mazao mengine yenye bei nzuri na soko la uhakika ndani na nje ya nchi. Mazao hayo ni pamoja na paprika, vanilla, pilipili manga, mbaazi, mbegu za mafuta na maua.

## Mazao ya viungo

**29.** Mazao ya viungo, hususan vanilla, paprika, pilipili manga na tangawizi yanastawi vizuri katika maeneo yanayopata mvua zaidi ya milimita 1000 kwa mwaka, wastani wa joto la nyuzi joto 25 $^{o}$C na unyevunyevu hewani wa wastani wa asilimia 60. Mikoa ya Kanda ya

Ziwa, Nyanda za Juu Kaskazini, Nyanda za Juu Kusini na mikoa ya Pwani ina hali ya hewa inayofaa kwa uzalishaji wa mazao ya viungo, Hata hivyo, uzalishaji wa mazao hayo bado ni wa chini sana. Baadhi ya matatizo yanayowakabili wakulima wa mazao ya viungo ni pamoja na ukosefu wa vipando na ujuzi wa uzalishaji. Katika mwaka wa 2002/2003, Wizara ilikusanya aina 10 za mazao hayo kutoka sehemu mbalimbali nchini na kuvipeleka kwenye Kituo cha Mafunzo na Utafiti cha Kilombero *(KATRIN)* kwa lengo la kuvifanyia tathmini na kuainisha aina zenye nasaba bora zinazofaa kulimwa kibiashara.

## III. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA KAZI KWA MWAKA WA 2002/2003

**30.** Mheshimiwa Spika, mwaka wa 2002/2003 ulikuwa mwaka wa kwanza wa kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo. Mpango wa Kilimo na Chakula kwa mwaka wa 2002/2003 ulilenga kuwekeza kwenye maeneo yaliyokuwa na uhusiano wa moja kwa moja na wakulima na ambayo yangekuwa na matokeo ya haraka. Mpango ulilenga kuongeza eneo linalomwagiliwa maji ili kuimarisha uhakika wa upatikanaji wa chakula na kuweka mifumo madhubuti ya upatikanaji wa mbegu bora, pembejeo nyingine na zana za kurahisisha kazi za kilimo na kupunguza upotevu wa mazao kabla na baada ya kuvuna. Aidha, mpango ulilenga kuimarisha huduma za ugani na mafunzo kwa wakulima na wataalamu kwa lengo la kumfikishia mkulima teknolojia bora za kilimo.

### Muundo wa Wizara

**31.** Wizara ilifanya mabadiliko katika mifumo ya utendaji na usimamizi wa Taasisi zilizo katika sekta ya Kilimo ili kuziwezesha kutekeleza majukumu ya asasi na taasisi hizo kwa ufanisi. Katika mabadiliko hayo, Idara mpya ya Umwagiliaji na Huduma za Ufundi ilianzishwa. Aidha, Idara za Maendeleo ya Utafiti na Mafunzo ziliunganishwa kuwa Idara moja ya Utafiti na Mafunzo.

**32.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2002/2003, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Maji na Maendeleo ya Mifugo, Ushirika na Masoko, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, iliandaa Mwongozo wa Kuandaa Mipango ya Kilimo ya Wilaya. Baadhi ya mipango hiyo itaanza kutekelezwa mwaka wa 2003/2004. Mipango hiyo ni muhimu kwani itahakikisha ushirikishwaji wa wananchi katika kupanga, kuteleza na kusimamia miradi yao ya maendeleo.

## IV. HUDUMA ZA UGANI

**33.** Mheshimiwa Spika, *mbinu shirikishi jamii* ni njia endelevu inayoshirikisha viongozi, wataalam na wakulima katika kuibua matatizo yanayowakabili wananchi katika kuendeleza huduma zao za kiuchumi na kijamii. Mbinu hiyo, huwezesha wakulima kupanga mipango yao na kuitekeleza kwa kutumia rasilimali zao na misaada mingine ikilazimu. Katika kutekeleza mbinu hiyo huundwa timu za kimkoa, kiwilaya, kata na vijiji zinazojumuisha viongozi na wataalam wa fani zinazohusika na maendeleo vijijini. Mbinu hiyo huweka bayana uwajibikaji wa viongozi, wataalam na wananchi katika kusimamia na kutekeleza mpango ulioandaliwa. Hivyo, *mbinu shirikishi jamii* huongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za ugani, usambazaji wa teknolojia mbalimbali kwa wakulima na matumizi ya rasilimali katika jamii. Kwa ujumla mbinu hiyo huchangia katika kuongeza tija na uzalishaji wa mazao, uhakika wa chakula katika kaya na kupunguza umaskini.

**34.** Ili kueneza matumizi ya *mbinu shirikishi jamii* nchini, mwaka wa 2002/2003, Wizara, ilifanya warsha ya Kitaifa ya mafunzo ya mbinu shirikishi jamii kwa Maafisa Viungo Utafiti na Ugani *(Research and Extension Liaison Officer)* wa Kanda, Maafisa Washauri wa Kilimo wa Mikoa na maafisa wa Kilimo na Mifugo wa Wilaya 538. Baada ya warsha hizo, maafisa hao waliwafundisha maafisa kilimo na mifugo waliopo katika ngazi ya kata na vijiji ambao nao waliwaelimisha wakulima 2,613. Aidha, Wizara iliwapatia mafunzo ya mbinu shirikishi jamii na Shamba Darasa wataalam 168 katika Vyuo vya Kilimo na Mifugo vya Mlingano, Morogoro na Mkindo. Baada ya kuhitimu, wataalam hao walitoa mafunzo hayo kwa wataalam wa ugani 1,130 waliopo vijijini. Aidha, vikundi 163 vya wakulima vyenye jumla ya wakulima 4,075 vilipata mafunzo ya Shamba Darasa.

**35.** Mheshimiwa Spika, ili kufikisha teknolojia bora za uzalishaji kwa wakulima, Wizara iliendelea kutumia vyombo vya habari hususan redio na majarida kuwaelimisha wakulima. Jumla ya vipindi vya redio 104 kuhusu mazao vilirushwa hewani na Redio Tanzania na makala kuhusu utaalam wa kilimo yalichapishwa katika majarida sita na kusambazwa kwa wakulima. Wizara iliandaa mada mbili za video kuhusu mbinu shirikishi jamii na kilimo cha uyoga ambazo zilionyeshwa kwa wakulima katika sikukuu ya Nane Nane na Siku ya Chakula Duniani ya mwaka wa 2002. Ili kuwawezesha wakulima kuendesha kilimo cha kibiashara, katika mwaka wa 2002/2003, Wizara iliandaa mafunzo yenye mwelekeo wa kilimo cha kibiashara kwa wakulima 200 juu ya mbinu za Kilimo bora cha korosho, tumbaku, kahawa na pamba.

## V. UTAFITI WA MAZAO YA KILIMO

**36.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2002/2003 huduma za utafiti zililenga kubuni teknolojia bora za uzalishaji wa mazao za kumwezesha mkulima kupata mavuno mengi na tija zaidi, na hivyo kumuongezea kipato na kumpunguzia umaskini. Teknolojia hizi ni pamoja na uzalishaji wa mbegu bora zenye sifa za kutoa mavuno mengi katika hali ya ukame, rutuba duni na zenye ustahimilivu wa visumbufu vya mimea. Aidha, teknolojia bora za kurutubisha udongo na kupambana na uharibifu wa ardhi zilichunguzwa, hususan katika maeneo yanayozalisha zao la Tumbaku, Mkoani Tabora. Ili kuhakikisha upatikanaji kwa wingi wa mbegu bora kwa wakulima nchini, mkazo uliwekwa katika kuzalisha kwa wingi mbegu mama za mazao mbalimbali kwenye Vituo vya Utafiti. Katika kutekeleza hayo, Wizara iliwashirikisha wakulima katika kutambua matatizo na kuainisha namna ya kuyatatua kwa kutumia mbinu *Shirikishi jamii.* Aidha, asilimia 55 ya majaribio yote yaliyofanyika msimu huu yalikuwa katika mashamba ya wakulima, ambalo ni ongezeko kubwa likilinganishwa na asilimia 36 tu miaka mitatu iliyopita.

**37.** Katika mwaka wa 2002/2003, ili kuhakikisha teknolojia zinazotolewa na vituo vya utafiti zinawafikia wakulima, Wizara ilianza kuzalisha kwa wingi mbegu mama *(breeder seed)* na za msingi *(foundation seed).* Aidha, wizara iliendelea kutafiti aina za mbegu zinazoweza kutoa mavuno mengi na zinazostahimili ukame, upungufu wa rutuba na visumbufu vya mimea.

### Kuzalisha na Kukuza Mbegu Mama za Mazao

**38.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003 Vituo vya Utafiti vilitoa mbegu mpya nane za mazao ya mpunga, mtama, maharage, mbaazi, soya, viazi vitamu na ngano. Uzalishaji wa mbegu hizo ulifanyika kikanda kama ifuatavyo:-

### Kanda ya Mashariki

**39.** **Kituo cha Ilonga** kilitoa aina mbili za mbegu mpya za mtama zinazojulikana kama *Wahi* na *Hakika* zinazovumilia magugu aina ya kiduha. Mbegu hizo ni kwa ajili ya Kanda za Kati na Ziwa. Kituo hicho pia kilitoa aina mpya ya mbaazi inayojulikana kama *"Mali"* ambayo inakomaa katika siku 270 na inaweza kuvunwa kwa misimu miwili. Mbegu mama za *Wahi, Hakika* na *Mali* zinaendelea kuzalishwa kwa wingi kwa ajili ya kupelekwa kwenye mashamba ya mbegu za msingi ili zizalishwe kwa wingi. Aidha, Kituo cha KATRIN kilichoko Ifakara, kilitoa mbegu mpya ya mpunga ijulikanayo kama SARO 5 yenye uwezo wa kuzaa tani tano kwa hekta na yenye ladha nzuri. Uzalishaji wa mbegu hiyo unaendelea katika mashamba ya Dakawa (hekta 20) na Kilangali (hekta 50). Tani 325 za mbegu ya SARO 5 zinatarajiwa kuvunwa na kuuzwa kwa wakulima kwa ajili ya kupandwa katika msimu wa 2003/2004.

**40.** **Kituo cha Kibaha** kilitoa aina mpya ya mbegu bora ya viazi vitamu inayojulikana kama *"Ukerewe"*. Mbegu hii ina uwezo wa kuzaa tani nane kwa hekta, inavumilia mashambulizi ya wadudu, na ina uwezo wa kuzaa wakati wa mvua za muda mfupi kwa mfano, mvua za vuli. Uzalishaji wa mbegu hii unaendelea katika vituo vya Kibaha, Dakawa na Ukiriguru na kwenye mashamba ya wakulima katika Kanda ya Kati na Ziwa.

### Kanda ya Nyanda za Juu Kusini

**41.** Katika mwaka wa 2002/2003, **Kituo cha Uyole** kwa mara ya kwanza katika kipindi cha miaka 30, kilitoa aina mpya ya mbegu ya soya ijulikanayo kama *"Soya-Uyole-I"*. Mbegu hii ina uwezo wa kutoa tani 1.5 hadi 1.8 kwa hekta kwenye mashamba ya wakulima na inategemewa kwamba upatikanaji wa mbegu hii utapunguza uhaba wa mbegu za soya uliokuwepo nchini. Aidha, kituo kilizalisha mbegu mpya ya maharage ijulikanayo kama "*Wanja*". Mbegu hii ina uwezo wa kutoa tani 1.0 hadi 1.5 kwa hekta kwenye mashamba ya wakulima na inalo soko zuri katika nchi za jirani. Kwa hiyo uzalishaji wa zao hili kwa wingi utapanua wigo wa mazao ya biashara kwa wakulima wa Nyanda za Juu Kusini.

### Kanda ya Kaskazini

**42.** **Kituo cha Selian**: Migomba ya asili inayolimwa sehemu nyingi nchini ina tija ndogo kati ya tani tano hadi saba za ndizi kwa hekta ikilinganishwa na tani 20 hadi 60 za ndizi kwa hekta kwa kutumia migomba bora. Ili kuongeza tija katika kilimo cha migomba na kufanya zao la ndizi liwe la biashara ndani na nje ya nchi, Kituo cha Selian kimekuwa kikitafiti na kuzalisha miche bora ya zao la migomba kwa kutumia *tissue culture.* Katika mwaka wa 2002/2003, Kituo cha Selian kilitoa miche 4,000 ya migomba bora kwa kutumia maabara. Aidha, ili kuongeza kasi ya uzalishaji wa miche ya migomba bora, Kituo kinatumia shamba la Maadira lililoko Tengeru. Shamba hilo lina uwezo wa kuzalisha miche 30,000 kwa mwaka. Miche hiyo husambazwa kwa wakulima waliopatiwa mafunzo ya kilimo bora cha migomba.

### Kanda ya Kusini

**43.** Katika mwaka wa 2002/2003 **Kituo cha Naliendele** kilizalisha mbegu bora za korosho kwa wingi kwa lengo la kukidhi mahitaji ya mbegu hizo nchini. Kati ya tani 6.4 za mbegu zilizotokana na mikorosho bora zilizozalishwa, tani 4.3 ziliuzwa kwa wakulima. Miche 3,080 ya mikorosho iliuzwa kwa wakulima wa mikoa ya Mtwara na Lindi.

## Kanda ya Ziwa

**44.** **Kituo cha Ukiriguru:** Katika mwaka wa 2002/2003, Kituo cha Ukiriguru kilizalisha mbegu mama za pamba aina ya UK 91 ili iweze kutumika kuzalisha mbegu za msingi na zilizothibitishwa. Tani nane za mbegu mama zinataratijwa kuvunwa kutoka katika shamba la Nkaziga. Aidha, Kituo cha Maruku kilichopo Mkoani Kagera kilizalisha miche bora ya kahawa aina ya *robusta* 10,000 kwa ajili ya kuwauzia wakulima.

## Majaribio ya Teknolojia

**45.** Mheshimiwa Spika, pamoja na kuzalisha mbegu bora za mazao katika vituo vya utafiti, Wizara ilifanya majaribio ya kilimo mseto, hifadhi ya ardhi na kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya kilimo. Kituo cha Tumbi kilifanya majaribio ya matumizi ya miti aina ya *Sesbania sp.* yenye uwezo wa kurutubisha udongo wa sehemu ilikopandwa. Miti hiyo ina uwezo wa kuongeza nitrogen kiasi cha kilo 30 – 40 kwa hekta kwa mwaka mahali ilipopandwa. Vilevile, imebainika kuwa matumizi ya kilimo mseto hupunguza athari za gugu aina ya *kiduha* kwenye kilimo cha mahindi. Kituo cha Mlingano kilifanya utafiti wa mazao jamii ya mikunde yenye uwezo wa kuhifadhi ardhi, kuongeza rutuba katika udongo, kudhibiti magugu na kutumika kama chakula cha mifugo. Matokeo ya mwisho ya tafiti hizo yanatarajiwa kupatikana katika mwaka wa 2003/2004.

## Taasisi za Utafiti wa Mazao ya Biashara

**46.** Mheshimiwa Spika, ili kuimairisha shughuli za utafiti wa mazao makuu ya biashara, taasisi za chai, kahawa na tumbaku zinaendelea kufanya utafiti kwa kuzingatia mahitaji ya wadau na zinawashirikisha wadau katika kugharamia uendeshaji wake.

**47.** **Taasisi ya Utafiti wa Chai (*Tea Reseach Institute of Tanzania – TRIT*):** Taasisi hii, ikishirikiana na wakulima wadogo wa chai na Maafisa Ugani wilayani Rungwe, imeweza kuongeza uzalishaji wa chai kutoka kilo 479 kwa hekta zilizozalishwa mwaka wa 2000, hadi kilo 1,043 kwa hekta mwaka wa 2001 na tani 2,208 kwa hekta mwaka wa 2002. TRIT iliendelea na utafiti kuhusu matumizi ya mbolea na maji katika kilimo cha chai. Aidha, taasisi ilianza kutathmini aina mpya za chai zilizoingizwa nchini kutoka Kenya.

**48.** **Taasisi ya Utafiti wa Kahawa (*Tanzania Coffee Research Institute – TACRI*):** Taasisi hii, iliyoanzishwa mwaka wa 2001, iliainisha aina 31 za mbegu chotara za kahawa ambazo zina sifa ya kustahimili mashambulizi ya ugonjwa wa chulebuni na kutu ya majani na hivyo kupunguza gharama za uzalishaji. Mbegu hizo sasa zinazalishwa kwenye vitalu ili zisambazwe kwa wakulima msimu wa 2003/2004.

**49.** Aidha, TACRI ilikamilisha uandaaji wa mkakati wa utafiti wa zao la kahawa kwa kipindi cha miaka mitano ijayo, kuanzia mwezi wa Julai, 2003. Mpango huo utakaogharamiwa na wadau wa sekta ya kahawa na Jumuia ya Ulaya, unalenga kuinua uzalishaji wa zao hilo kwa kuwapatia wakulima teknolojia bora za uzalishaji.

**50.** **Taasisi ya Utafiti wa Tumbaku (*Tobacco Research Institute of Tanzania – TORITA*):** Taasisi hii pamoja na kuendelea kufanya majaribio ya matumizi ya mbolea na mbegu mpya za tumbaku, iliendesha mafunzo juu ya utunzaji bora wa vitalu vya tumbaku na kilimo bora cha tumbaku kwa maafisa ugani wa Wilaya za Chunya (10), Namtumbo (10), Songea (5) na Mpanda (10). Jumla ya wakulima 120 mkoani Tabora walipewa mafunzo ya kilimo bora cha tumbaku. Kutokana na mafunzo haya, ubora wa zao la tumbaku unatarajiwa kuongezeka.

### Ukarabati wa Vituo vya Utafiti

**51.** Mheshimiwa Spika, ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za utafiti, katika mwaka wa 2002/2003, Wizara ilikarabati ofisi, maabara na baadhi ya nyumba za wafanyakazi katika vituo vya utafiti vya Ukiriguru, Maruku, KATRIN, Uyole, Selian, Tumbi na Mlingano na kuvipatia vifaa vya kisasa vya kufanyia utafiti. Wizara pia ilijenga miundombinu ya umwagiliaji maji mashambani katika vituo vya Uyole, Ilonga, Selian na Tumbi ili viweze kuongeza kasi ya uzalishaji wa mbegu kwa kupunguza muda kati ya zao moja na lingine. Aidha, ukarabati na ujenzi wa maabara za kuzalisha mimea *(tissue culture labs)* ulikamilika katika vituo vya Mikocheni, Uyole na Ukiriguru. Madawa yatakayotumika katika maabara hizo yaliagizwa kutoka nje na yanatarajiwa kuwasili nchini katika mwaka wa 2003/2004.

## VI. KILIMO CHA UMWAGILIAJI MAJI MASHAMBANI

**52.** Mheshimiwa Spika, lengo la Wizara ya Kilimo na Chakula kwa mwaka wa 2002/2003 lilikuwa kupanua eneo linalolimwa kwa kumwagilia maji mashambani ili kuliongezea Taifa uzalishaji wa mazao na kuboresha usalama wa chakula. Jumla ya hekta 8,995 ziliendelezwa kwa Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani na kufanya eneo lote linalolimwa kuwa hekta 200,895 likilinganishwa na hekta 191,900 zilizolimwa mwaka 2001/2002. Wizara itaendelea na juhudi hizo katika miaka ijayo kuhakikisha kwamba eneo lote linalofaa sana kwa Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani (hekta 2.3 milioni) kama ilivyoainishwa katika mpango kabambe wa Kilimo cha Umwagiliaji maji mashambani linaendelezwa.

### Mpango Kabambe wa Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani

**53.** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo na Chakula, kwa kushirikiana na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (JICA), imekamilisha maandalizi ya Sehemu ya Kwanza ya Mpango Kabambe wa Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani. Mpango huo umeonyesha kwamba kuna **hekta milioni 2.3 zenye uwezekano mkubwa wa kuendelezwa** (*high development potential*). Aidha, zipo **hekta milioni 4.8 zenye uwezekano wa wastani wa kuendelezwa** (*medium development potential*) na **hekta milioni 22.3 zenye uwezekano mdogo wa kuendelezwa** (*low development potential*). **Kwa jumla, Taifa lina hekta milioni 29.4 zinazofaa kuendelezwa kwa kilimo cha umwagiliaji maji mashambani**.

**54.** Kutokana na uchunguzi huo, ni dhahiri kuwa kuna uwezekano mkubwa sana wa kuendeleza kilimo cha umwagiliaji maji mashambani hivyo kuliwezesha Taifa kuboresha usalama wa chakula kwa kuongeza uzalishaji wa nafaka, hususan mpunga. Aidha, uzalishaji wa mazao yenye thamani kubwa kama mboga, matunda na maua ungeongezeka.

**55.** Ripoti ya Mpango Kabambe wa Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani imeandaliwa na nakala zake zimesambazwa katika Halmashauri zote za wilaya. Halmashauri zenye maeneo yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji maji mashambani yaliyoainishwa katika ripoti hiyo zinapaswa ziitumie ripoti hiyo kuandaa na kutekeleza miradi ya umwagiliaji maji mashambani.

### Ukarabati wa Skimu za Umwagiliaji Maji Mashambani

**56.** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo na Chakula imeweka mkazo katika ukarabati wa Skimu za zamani za umwagiliaji maji mashambani zenye gharama nafuu na urahisi wa kutekeleza katika mwaka wa 2002/2003, skimu 12 zenye jumla ya hekta 3,936

zilikarabatiwa. Skimu hizo ni Musa Mwinjanga, Hai (hekta 641), Bugorora, Ukerewe (hekta 200), Kalemela, Magu (hekta 20), Kalenga, Iringa (hekta 240), Mvumi, Kilosa (hekta 260), Mbarika, Misungwi (hekta 45), Muhwazi, Kibondo (hekta 100), Katuka, Sumbawanga (hekta 100), Ruvu, Bagamoyo (hekta 720), Kitivo, Lushoto (hekta 490) na Shamba la uzalishaji mbegu Kilangali Kilosa (hekta 1,020). Aidha, bwawa linalotumika kumwagilia skimu ya Kitere, Mtwara (hekta 100) lilikarabatiwa.

**Mradi wa Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani katika Mabonde ya Mito Pangani na Rufiji** ***(River Basin and Smallholder Irrigation Improvement Project – RBSIIP)***

**57.** Katika mwaka wa 2002/2003 Wizara iliendelea kutekeleza Mradi wa Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani katika Mabonde ya Mito Pangani na Rufiji. Mradi huu unaogharamiwa na Serikali ya Tanzania, **Benki ya Dunia** na wakulima wenyewe, uliendelea na ujenzi wa skimu nne zenye jumla ya hekta 1,169. Skimu hizo ni Mapogoro, Iringa (hekta 350), Nyamahana, Iringa (hekta 109), Kivulini, Mwanga (hekta 410) na Longoi, Hai (hekta 300). Skimu hizi, pamoja na skimu 11 zilizokamilishwa mwaka wa 2001/2002, zimeendeleza eneo lenye jumla ya hekta 5,059 katika Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Tanga, Iringa na Mbeya. Aidha, jumla ya wakulima 440 kutoka katika skimu 15 zilizokarabatiwa chini ya mradi huu walipewa mafunzo juu ya usimamizi na uendeshaji wa skimu. Mradi ulianzisha mashamba madogo manne yenye eneo la hekta tano kila mmoja ambayo yalizalisha tani 100 za mbegu ya mpunga aina ya SARO 5. Mashamba haya yako katika skimu za Igomelo (Mbarali), Luganga (Iringa), Lekitatu (Arumeru) na Mombo (Korogwe).

**Programu Husishi ya Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani** ***(Participatory Irrigation Development Programme – PIDP)***

**58.** Katika mwaka wa 2002/2003, Wizara iliendeleza teknolojia rahisi ya uvunaji maji kwa njia ya majaruba na uchimbaji wa visima vifupi katika maeneo kame ili kuongeza uzalishaji wa zao la mpunga. Kazi hii ilifanyika chini ya Programu Husishi ya Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani. Programu hii inayogharamiwa na Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Kilimo (IFAD), Serikali ya Ireland, Mpango wa Chakula Duniani (WFP) na Serikali ya Tanzania inalenga kuendeleza hekta 7,200 itakapokamilika mwaka wa 2005/2006. Katika mwaka wa 2002/2003, skimu 21 zenye hekta 4,669 katika wilaya sita za Dodoma Vijijini, Manyoni, Nzega, Shinyanga, Kwimba na Babati zilifanyiwa usanifu na ujenzi wake umeanza kwa kushirikiana na wilaya husika. Orodha ya skimu zote na hatua iliyofikiwa katika utekelezaji imeonyeshwa katika kiambatanisho Na. 2.

**59.** Kazi nyingine zilizofanywa ni kufundisha maafisa ugani 37, mafundi sanifu wa umwagiliaji 12 na wakulima 6,509 mbinu za kisasa za kilimo cha mpunga. Mafanikio ya juhudi hizo ni pamoja na ongezeko la uzalishaji wa mpunga kutoka wastani wa tani 2.4 kwa hekta mwaka wa 1999/2000 hadi tani 5.6 kwa hekta mwaka wa 2002/2003. Aidha, Programu imekamilisha ujenzi wa visima vifupi 24 kwa ajili ya kumwagilia mazao ya bustani na vitalu vya mbegu za mpunga.

**Mradi wa Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani chini ya Programu ya Kusaidia Sekta ya Kilimo** ***(Agricultural Sector Project Support Project – ASPS)***

**60.** Mradi huu unagharamiwa na Serikali za Tanzania na Denmark kwa lengo la kuendeleza skimu tano za kilimo cha umwagiliaji maji mashambani zenye jumla ya hekta

3,830 kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya husika. Skimu hizo ni Lumuma, Kilosa (hekta 960); Nyanzwa (hekta 760) na Irindi, Iringa (hekta 610); Utengule Usongwe, Mbeya (hekta 600) na Naming'ong'o, Mbozi (hekta 1,000). Katika mwaka wa 2002/2003, ujenzi wa skimu ya Lumuma ulikamilika. Usanifu wa skimu nne zilizobaki umefanyika ili ujenzi uanze katika mwaka 2003/2004. Aidha, mafunzo yalitolewa kwa wakulima 4,325 juu ya kuunda na kuimarisha vikundi vya Umoja wa Wamwagiliaji Maji Mashambani na matumizi bora ya maji.

### Vyama vya Umwagiliaji Maji Mashambani

**61.** Wizara ya Kilimo na Chakula ilishiriki katika kuanzisha vyama vya umwagiliaji maji mashambani katika skimu 6 za Bagamoyo na Ruvu (Pwani), Lumuma (Kilosa), Balili (Bunda), Ochuna (Tarime), na Buswahili (Musoma). Aidha, mafunzo yalitolewa kwa viongozi 36 wa vyama vya umwagiliaji maji mashambani katika nyanja ya usimamizi na uendeshaji wa skimu za umwagiliaji maji mashambani.

### Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji *(Participatory Agricultural Development and Empowerment Project – PADEP)*

**62.** Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji umeanza kutekelezwa rasmi kuanzia mwezi wa Mei, 2003. Hapo awali mradi huu ulijulikana kwa jina la Mradi wa Kuongeza Rutuba kwenye Udongo na Tija katika Kilimo *(Soil Fertility Recapitalization and Agricultural Intensification Project- SOFRAIP)*. Hii imetokana na umuhimu wa kusisitiza dhana ya ushirikishaji jamii na kujenga uwezo na ujasirimali wa wakulima na wafugaji katika kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo ya kilimo na ufugaji. Mradi unalenga kuongeza uzalishaji na tija ya kilimo na hivyo kupunguza umaskini. Mradi huu utatekelezwa katika wilaya 28 za Tanzania Bara na Visiwani.

**63.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2002/2003 mradi umetekelezwa kwa majaribio katika Wilaya za Hai na Morogoro Vijijini. Shughuli zilizofanyika katika Wilaya hizo zimeonyesha mafanikio katika kuwashirikisha wakulima na wafugaji kwa kuyatambua matatizo na kutafuta mbinu za kuyatatua kwa kutumia raslimali walizonazo. Watekelezaji wamejifunza kuwa kwa **kuwawezesha** wakulima na wafugaji kutambua fursa zilizopo, miradi ya maendeleo ya kilimo inaweza kutekelezwa na kusimamiwa vizuri katika ngazi ya kijiji. Pamoja na kutekeleza mradi, marekebisho muhimu yamefanyika kwa kuzingatia matokeo yaliyopatikana kwa lengo la kuongeza ufanisi katika kipindi cha utekelezaji. Aidha, maandalizi ya utekelezaji yameendelea kufanyika katika Wilaya za Iringa, Singida, Hanang, Arumeru, Masasi na Nachingwea. Maeneo haya yataanza kutekeleza shughuli za mradi katika mwaka wa 2003/2004.

**64.** Wilaya zitatakiwa kuteua vijiji kulingana na fursa zilizopo katika vijiji hivyo, matatizo yaliyopo katika kuendeleza kilimo, mihadi (*commitment*), kuchangia asilimia 10 ya gharama za uwezeshaji (*capacity building*) na hamasa ya wilaya katika kuleta maendeleo ya kilimo kwa utaratibu wa mbinu *shirikishi jamii*. Viongozi wote hususan wa wilaya wanatakiwa kuwaelewesha wananchi kuhusu uendeshaji wa mradi ili waweze kutambua maeneo ambayo yataleta mabadiliko katika kukabiliana na matatizo yanayoikabili sekta ya kilimo.

## VII. PEMBEJEO NA ZANA ZA KILIMO

**65.** Mheshimiwa Spika, matumizi ya pembejeo na zana bora za kilimo ambazo ni muhimu sana katika kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya kilimo, bado ni madogo. Matumizi ya zana na pembejeo yameshuka hasa baada ya kuanza kwa sera za soko huru ambapo utaratibu uliokuwepo awali wa upatikanaji, ugharamiaji na usambazaji wa pembejeo za kilimo ulivurugika. Ili kilimo kikue kwa kasi itakayotuwezesha kupambana na umasikini, ni lazima matumizi ya zana na pembejeo katika uzalishaji wa mazao ya kilimo, yaongezeke.

**66.** Kuanzia msimu wa 2002/2003, Wizara imeweka mfumo wa kuwawezesha waagizaji na wasambazaji wa pembejeo na zana za kilimo kupata mikopo kutoka kwenye Mfuko wa Taifa wa Pembejeo kupitia benki kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utoaji wa mikopo. Mfumo huo unazihusisha Halmashari za Wilaya katika kubaini mahitaji, wasambazaji na waagizaji wa pembejeo. Halmashauri za Wilaya pia zinawajibika kusimamia matumizi ya pembejeo na zana zinazotokana na mikopo hiyo. Wizara inaweka mkazo katika kuhamasisha sekta binafsi kushiriki katika uagizaji na usambazaji wa pembejeo na zana bora kwa wingi na kwa wakati unaotakiwa.

### Mbolea na Madawa

**67.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2002/2003, makadirio ya mahitaji ya mbolea nchini yalikuwa tani 185,500. Hadi kufikia mwezi wa Mei 2003, kiasi cha tani 111,025.2, za mbolea, sawa na asilimia 60 ya mahitaji zilipatikana na kusambazwa kwa wakulima. Upungufu ulitokana na baadhi ya makampuni kutoagiza mbolea kwa wingi kutokana na wakulima kutumia kiasi kidogo cha mbolea. Hadi kufikia mwezi wa Mei 2003, tani 83,393 zilikuwa zimetumika. Matumizi madogo ya mbolea yametokana na bei kubwa ya mbolea na ukame uliojitokeza. Aidha, mahitaji ya viuatilifu aina ya unga yalikuwa tani 21,000 na vya aina ya maji yalikuwa lita milioni 4.0. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Mei, 2003, upatikanaji wa madawa aina ya unga ulikuwa tani 12,000 na lita milioni 2.125 za madawa ya maji.

### Mbegu Bora

**68.** Mheshimiwa Spika, makadirio ya mahitaji ya mbegu bora kwa mwaka wa 2002/2003 yalikuwa ni tani 30,000. Upatikanaji wa mbegu bora ulifikia tani 10,426 sawa na asilimia 35 ya mahitaji ya mbegu bora nchini. Mashamba ya mbegu ya Serikali yalichangia tani 267 za mbegu za msingi, sawa na asilimia 1.0 ya mahitaji. Chini ya utaratibu wa mfumo wa kuzalisha mbegu kwa kutumia wakulima wadogo vijijini, tani 573 zilizalishwa,sawa na asilimia 2.0 ya mahitaji. Makampuni binafsi ya mbegu yalizalisha tani 9,586 sawa na asilimia 32 ya mahitaji.

**69.** Katika msimu wa 2002/2003, mashamba ya Dabaga, Kilangali, Msimba, Arusha na Mwele na Vituo vya Utafiti yalilenga kulima jumla ya hekta 690 ambazo zingezalisha tani 875.4 za mbegu bora za nafaka, mikunde na mbegu za mafuta. Hadi kufikia mwezi wa Mei, 2003, jumla ya hekta 670 ambazo ni asilimia 97, zilikuwa zimelimwa na kupandwa na zinatazamiwa kuzalisha tani 1,047 za mbegu hizo.

### Sheria Mpya ya Mbegu

**70.** Muswada wa Sheria mpya ya mbegu umeandaliwa na unatarajiwa kuwasilishwa na kujadiliwa katika Kikao cha Bunge cha mwezi wa Oktoba, 2003. Sheria hiyo itazingatia mambo makuu yafuatayo:

- Kuwa na sheria mpya ya mbegu itakayokidhi mazingira ya soko huru;
- Sekta binafsi kuruhusiwa kisheria kufanya shughuli za kuzalisha, kuagiza, kuuza ndani na nje ya nchi, kuandaa, kusambaza, na hata kutangaza biashara ya mbegu;
- Kuwataka wazalishaji na wauzaji wa mbegu kuzalisha au kuuza mbegu zilizosajiliwa tu;
- Kudhibiti ubora wa mbegu zinazozalishwa na zinazoingizwa nchini; na
- Kuanzisha kisheria ofisi ya Msajili wa Mbegu.

### Wakala wa Mbegu wa Serikali

**71.** Mheshimiwa Spika, kutokana na kusambaratika kwa Kampuni ya Mbegu ya TANSEED, Wizara imebuni utaratibu mpya wa kuzalisha, kusambaza na kusimamia uagizaji wa mbegu kutoka nje ya nchi. Vituo vya Utafiti vitasimamia uzalishaji wa mbegu mama na za msingi wakati mashamba ya mbegu ya Serikali na watu binafsi watakaopewa mikataba ya kuzalisha mbegu, watazalisha mbegu iliyothibitishwa *(certified seed*). Vijiji vitaendelea kuzalisha mbegu iliyoidhinishwa *(quality declared seed)*. Ili kusimamia uzalishaji wa mbegu nchini na uagizaji wa mbegu kutoka nje ya nchi, Serikali inafanya maandalizi ya kuanzisha Wakala wa Mbegu wa Taifa. Maandalizi yalianza mwaka wa 2003 na yatakamilika mwaka wa 2004.

### Zana za Kilimo

**72.** Mheshimiwa Spika, mwaka wa 2002/2003, jumla ya matrekta makubwa 274, matrekta madogo ya mkono 75, majembe ya kukokotwa na wanyamakazi 19,319 na majembe ya mkono 2,107,550 yaliingizwa nchini. Eneo linalolimwa na wanyamakazi ni asilimia 20 na lile linalolimwa kwa matrekta ni asilimia 10 ya eneo lote linalolimwa nchini. Taarifa hizi zinaonyesha kuwa kilimo chetu bado kinategemea zaidi jembe la mkono ambalo linarudisha nyuma uwezo wa wakulima kuongeza maeneo wanayolima.

**73.** Mheshimiwa Spika, katika kuhimiza matumizi ya matrekta, Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kupitia Halmashauri za Wilaya imeuza matrekta madogo ya mkono 83 kwa wakulima binafsi 67 na vikundi vya wakulima 16. Matrekta haya ni sehemu ya matrekta madogo 170 yaliyoingizwa nchini chini ya Mpango Maalum wa Kuongeza Uzalishaji wa Mazao (KR II) unaofadhiliwa na Serikali ya Japan. Ili kuwapa wakulima unafuu wa bei, Wizara ilipunguza bei ya matrekta hayo, kutoka shilingi milioni 4.425 hadi shilingi milioni 2.5 kwa trekta moja. Mafunzo juu ya matumizi ya matrekta hayo yametolewa kwa maafisa ugani 37 na wakulima 130 kutoka mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Iringa, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Lindi, Ruvuma na Tanga.

**74.** Katika kuendeleza kilimo cha wanyamakazi, jumla ya vituo vya wanyamakazi 20 katika mikoa ya Mwanza (1), Shinyanga (1), Singida (1), Dodoma (2), Iringa (3), Morogoro (1), Mbeya (2), Manyara (1), Tanga (1), Tabora (1), Rukwa (2), Mara (1), Pwani (1), Mtwara (1) na Kilimanjaro (1) vimefanyiwa ukarabati ili vitoe mafunzo kwa vitendo ya matumizi ya wanyamakazi. Maafisa ugani 520 na wakulima 7,395 walipatiwa mafunzo katika nyanja hiyo.

## VIII. MATUMIZI BORA YA ARDHI

**75.** Mheshimiwa Spika, sehemu kubwa ya nchi yetu inakabiliwa na mmomonyoko wa udongo unaosababishwa na kuondolewa kwa uoto wa asili na kilimo kisichohifadhi ardhi.

Mmomonyoko huo, umesababisha sehemu nyingi kukabiliwa na hatari ya kupoteza rutuba na hata maeneo ya uzalishaji. Hali hiyo ipo katika mikoa yote ya Tanzania Bara ijapokuwa mikoa inazidiana kwa viwango vya uharibifu. Mikoa inayoongoza kwa tatizo la mmomonyoko wa ardhi ni ya Kilimanjaro, Arusha, Singida, Manyara, Dodoma, Tanga, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Iringa, Kagera, Tabora, Shinyanga, Kigoma, Mara, Pwani, Mtwara, Ruvuma na Rukwa. Hali hiyo isipodhibitiwa inaweza kusababisha kuenea kwa hali ya jangwa, kama inavyojidhihirisha katika maeneo ya Mombo mkoani Tanga na tambarare za mkoa wa Kilimanjaro hususan maeneo ya Hedaru, Mwanga na Same. Aidha, mmomonyonyo mkubwa wa udongo uliopo katika wilaya za Monduli mkoani Arusha na wilaya za Karatu na sehemu kubwa za mkoa wa Dodoma tayari umesababisha upotevu wa maeneo ya kilimo na malisho. Ili kuhifadhi udongo, hatua za haraka zinapaswa kuchukuliwa. Kwa bahati nzuri, mbinu za kukabiliana na mmomonyoko wa udongo zinafahamika na wananchi wengi. Mbinu hizo ni pamoja na kulima kilimo cha matuta na makinga maji. Mbinu nyingine ni kupanda miti au mimea mingine ya kuzuia kasi ya maji na upepo. Utekelezaji wa mbinu hizi unahitaji kupewa msukumo mkubwa na utekelezaji wake unapaswa utekelezwe sehemu zote nchini.

**76.** Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na tatizo hilo, katika mwaka wa 2002/2003, kwa kuanzia, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Handeni mkoani Tanga, imeainisha maeneo ya ardhi kwa ajili ya shughuli za kilimo, malisho, misitu, makazi na kuhakiki mipaka ya vijiji 43. Ramani zinazoonyesha aina za udongo, rasilimali mbalimbali zilizomo, na mapendekezo ya mpango wa matumizi bora ya ardhi wilayani humo zimeandaliwa. Aidha, Wizara ilitoa mafunzo ya nadharia na vitendo kwa maafisa ugani 190 katika ngazi za wilaya na vijiji na wakulima wakufunzi 80 kutoka wilaya 22. Mafunzo hayo yaliandaliwa kuwapa utaalam maafisa ugani na wakulima mbinu endelevu za matumizi ya ardhi.

## IX. MFUKO WA PEMBEJEO

**77.** Mheshimiwa Spika, ili kuboresha upatikanaji wa pembejeo na zana kwa wakulima na kuweka mfumo endelevu wa kugharamia ununuzi wa pembejeo, kuanzia mwaka wa 1995/1996 hadi 1998/1999, Mfuko wa Pembejeo ulitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 5.8. Tangu mwaka wa 1995/1996 hadi mwezi wa Mei, 2003, Mfuko umekuwa ukifuatilia wadaiwa na jumla ya shilingi bilioni 2.61 zimerejeshwa. Juhudi za kufuatilia ulipaji wa madeni yaliyobakia zinaendelea ikiwa ni pamoja na kuuza dhamana za wadaiwa ili kuhakikisha kwamba mikopo iliyobaki inarejeshwa.

**78.** Katika mwaka wa 2002/2003, Mfuko wa Pembejeo ulianza tena kutoa mikopo kwa wauzaji na wasambazaji wa pembejeo kupitia mabenki na kwa kuhusisha Halmashauri za Wilaya. Mfuko wa Pembejeo umeingia mikataba na Benki ya Exim na Benki ya Ushirika ya Kilimanjaro ambapo mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 2.05 imetolewa. Benki ya Ushirika ya Kilimanjaro ilitoa mikopo yenye thamani ya Shilingi milioni 126.5 na Benki ya Exim ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 1.93 kwa wasambazaji wa pembejeo.

**79.** Kuanzia mwaka wa 2002/2003, Mfuko wa Pembejeo umeingia mikataba baina yake na Benki ya Ushirika ya Wakulima wa Kagera, Benki ya Wananchi ya Mufindi, Benki ya Kimataifa ya Malaysia (T) Limited na Shirikisho la Vyama vya Ushirika vya Kuweka na Kukopa Tanzania *(SCULT (1992) LTD)* ili kupanua wigo wa utoaji wa mikopo nchini.

Mikopo kupitia Benki na Vyama hivyo inatazamiwa kuanza kutolewa katika msimu wa 2003/2004.

## X. UDHIBITI WA VISUMBUFU VYA MIMEA NA MAZAO

**80.** Mheshimiwa Spika, Wizara inatilia mkazo udhibiti wa visumbufu vya mimea na mazao ili kupunguza athari inayoweza kutokea kwenye maeneo yenye milipuko ya visumbufu hivyo. Inakadiriwa kwamba kila mwaka, visumbufu vya mimea na mazao husababisha uharibifu wa zaidi ya asilimia 30 ya mazao yanayozalishwa nchini. Katika udhibiti wa visumbufu vya mimea na mazao, Wizara hutumia viuatilifu, udhibiti kwa njia ya kibaolojia, udhibiti sango *(cultural control)* na udhibiti husishi. Aidha, katika msimu wa 2002/2003, Wizara ilijiimarisha ili kukabiliana na milipuko ya visumbufu mara inapotokea kwa kuwa tunao uhakika wa kupata huduma za ndege za kunyunyizia dawa kutokana na kulipa kikamilifu michango kwa Mashirika ya Kimataifa ya Udhibiti wa Visumbufu. Aidha, uwezo wa Wizara wa kununua na kusambaza viuatilifu umeimarishwa.

**81.** Katika mwaka wa 2002/2003, Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa, wakulima na taasisi mbalimbali ilipambana na milipuko ya visumbufu vya mimea na mazao mara tu ilipojitokeza. Visumbufu hivyo ni pamoja na ndege waharibifu wa nafaka aina ya kwelea kwelea na kasuku, nzige, viwavijeshi, panya na magonjwa mbalimbali ya mimea. Milipuko hiyo ilidhibitiwa katika mikoa 19 kati ya mikoa 21 ya Tanzania Bara. Hadi kufikia mwezi wa Aprili 2003, Wizara ilifanikiwa kuwadhibiti *Kwelea kwelea* waliovamia mashamba ya nafaka kwenye vijiji 30 katika mikoa ya Dodoma, Kilimanjaro, Mbeya na Singida. Katika kipindi hicho mlipuko wa ndege aina ya kasuku uliovikumba vijiji 17 vya mkoa wa Singida na kushambulia mazao ya alizeti, uwele, ulezi, mtama, mahindi na mpunga ulidhibitiwa.

**82.** Aidha, katika mwaka wa 2002/2003, ulitokea mlipuko wa nzige wekundu katika mbuga za Wembere (Tabora); Bonde la mto Malagarasi (Kigoma) na Iku Katavi (Rukwa). Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Kudhibiti Nzige Wekundu na Halmashauri za Wilaya husika ilidhibiti makundi 50 ya nzige kwenye mbuga za Iku Katavi, Malagarasi na Wembere. Kama makundi haya yasingedhibitiwa mapema yangevamia mashamba na kusababisha hasara kubwa.

**83.** Katika mwaka wa 2002/2003, mikoa ya Mtwara, Dar es Salaam, Iringa, Manyara, Morogoro, Singida, Tanga na Tabora ilivamiwa na viwavi jeshi. Wadudu hao walishambulia hekta 9,200 za mashamba ya mahindi, mpunga, mtama, uwele na maeneo ya malisho. Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine, ilikabiliana na tatizo hilo ambapo lita 21,500 za dawa zilitumika kudhibiti milipuko hiyo. Juhudi hizo ziliokoa asilimia 90 za mazao na malisho yaliyoshambuliwa.

**84.** Katika mwaka wa 2002/2003, milipuko ya panya ilitokea katika maeneo mbalimbali nchini na kusababisha uharibifu mkubwa wa mazao mashambani na kwenye maghala. Mikoa iliyokumbwa na milipuko hiyo ni Pwani (Bagamoyo), Lindi (Nachingwea, Ruangwa na Kilwa), Morogoro (Mvomero na Morogoro Vijijini), Mbeya (Chunya) na Mtwara (Masasi). Mazao yaliyoshambuliwa na panya hao ni mahindi, ngano, pamba, karanga, dengu, vitunguu, mpunga, khartamu, muhogo na nyanya. Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kushirikiana na Halmashauri za wilaya na wakulima, ilidhibiti milipuko hiyo kwa kutumia jumla ya kilo 1,430 za sumu ya panya.

### Udhibiti wa Ugonjwa wa Muhogo (Batobato)

**85.** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo na Chakula iliendelea kudhibiti ugonjwa wa muhogo uitwao batobato, katika Kanda ya Ziwa ambao uligunduliwa hapa nchini mwaka wa 1997. Ugonjwa wa batobato huenezwa na nzi mweupe na kwa njia ya vipando vya muhogo vyenye ugonjwa. Njia za udhibiti wa ugonjwa huo ni pamoja na kuweka eneo lililoathirika chini ya karantini, kung'oa na kuchoma muhogo ulioathirika, kupanda aina za muhogo zenye ukinzani dhidi ya batobato na palizi la mara kwa mara la mashamba ya muhogo.

**86.** Ili kudhibiti ueneaji wa ugonjwa wa batobato nje ya eneo lililoathirika, mwaka wa 1999, Serikali iliuweka mkoa wa Kagera chini ya karantini. Aidha, wakulima mkoani Kagera wametekeleza kikamilifu agizo la karantini. Kutokana na juhudi za wakulima na viongozi katika mkoa huo, ugonjwa wa batobato umepungua kwa kiasi kikubwa mkoani Kagera. Katika mwaka wa 2002/2003, Wizara ilizalisha mbegu stahimilivu 3,741,225 na kuzisambaza katika mikoa ya Kagera, Mwanza na Mara kwa ajili ya kueneza aina mpya za muhogo zenye ukinzani dhidi ya ugonjwa wa batobato. Ugonjwa huo umeanza kuenea katika wilaya za Kibondo, Bukombe na Sengerema. Wizara inaandaa utaratibu wa kuweka wilaya hizo chini ya karantini ya ugonjwa wa batobato, ili kuzuia utoaji wa mimea ya muhogo nje ya wilaya zilizoathirika na kuwataka wakulima kung'oa na kuchoma mihogo yenye ugonjwa huo.

### Udhibiti wa Ugonjwa wa Mnyauko wa Kahawa

**87.** Mheshimiwa Spika, uchunguzi uliofanywa na Wizara katika maeneo yote yanayolima kahawa umeonyesha kwamba ugonjwa wa mnyauko wa kahawa *(fusarium wilt)* upo katika mkoa wa Kagera peke yake. Ugonjwa huu umeathiri zao la kahawa aina ya *robusta* katika wilaya za Bukoba, Karagwe na Muleba. Katika mwaka wa 2002/2003, Wizara imeliweka eneo lote lenye ugonjwa wa mnyauko chini ya karantini. Wizara kwa kushirikiana na Shirika la *Commonwealth Agricultural Bureau* na Taasisi ya Utafiti wa Kahawa (*TACRI*) inaendelea kudhibiti na kuzuia kuenea kwa ugonjwa huo.

### Udhibiti wa visumbufu vya Migomba

**88.** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo na Chakula iliendelea kushirikiana na mradi uliokuwa chini ya Programu ya *Kagera Community Development* (KCDP) kudhibiti magonjwa ya zao la migomba na visumbufu vinavyoathiri zao hilo katika Kanda ya Ziwa. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2003, jumla ya miche stahimilivu 71,359 ya aina 25 za migomba iliingizwa nchini kutoka Ubelgiji. Kwa kutumia miche hiyo jumla ya miche 1,509,000 imezalishwa na kusambazwa kwa wakulima.

### Udhibiti Husishi wa Visumbufu vya Mimea

**89.** Katika mwaka wa 2002/2003, Wizara iliendelea kuelimisha wakulima juu ya mbinu endelevu na rahisi za udhitibiti wa visumbufu vya mimea na mazao husan mbinu ya udhibiti husishi na udhibiti kibaolojia. Wakulima wa mazao ya pamba, viazi vitamu, mahindi na mtama, kahawa, migomba na mazao jamii ya mboga mboga katika Kanda ya Ziwa na Nyanda za Juu Kaskazini walipatiwa mafunzo ya udhibiti husishi wa visumbufu vya mazao hayo.

**90.** Katika mwaka wa 2002/2003, jumla ya wadudu maadui 10,000 wa kidunga'ta wa muhogo walisambazwa katika mikoa ya Mwanza na Mara ili kukabiliana na mashambulizi ya kidung'ata wa muhogo. Wadudu maadui wa funza wa mabua ya mazao ya nafaka

*(Cotesia flavipes)* walisambazwa katika mikoa ya Pwani, Morogoro na Mara ili kudhibiti mashambulizi ya funza hao. Mbawakavu 340, maadui wa viwavi wa kipepeo *(diamond backmoth)* vinavyo shambulia zao la kabichi, waliingizwa nchini kutoka Kenya na kusambazwa mkoani Arusha. Wizara inaendelea kutathmini uwezo wa mbawakavu hao kudhibti viwavi wa vipepeo hao wanaoshambulia zao la kabichi.

**91.** Wizara ya Kilimo na Chakula iliendelea kuzalisha na kusambaza *mbawakavu* wanaodhibiti gugu maji katika vituo 12 vilivyoko katika bonde la Ziwa Viktoria kwa ajili ya udhibiti wa gugumaji Ziwani humo kwa njia ya kibiolojia. Aidha, uvunaji na usambazaji wa mbawakavu kutoka kwenye vituo hivyo uliendelea katika maeneo ya Ziwa Viktoria na mito ya Kagera, Mara, Kanoni na Kahororo na kwenye mabwawa ya Nguliati (Bariadi) na Bukabwa (Musoma).

**92.** Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka wa 2002, jumla ya hekta 1,867 za gugumaji katika mwambao wa Ziwa Viktoria lilikuwa limedhibitiwa. Udhibiti huo ni sawa na asilimia 93 ya gugumaji lililokuwepo awali. Udhibiti wa gugumaji umewezesha maeneo muhimu 530 yaliyokuwa yamezibwa na gugumaji kusafishwa. Pamoja na mafanikio hayo, tatizo la gugumaji linaendelea kuwepo katika Ziwa Viktoria kutokana na kuingia kwa gugu hilo kupitia mto Kagera kutoka nchi ya Rwanda ambako kuna gugu hilo. Wizara imetoa mafunzo kwa wataalam wa Rwanda ili waanze kazi ya udhibiti. Aidha, Vituo vinne vya kuzalisha mbawakavu vimeanzishwa nchini Rwanda kwa ajili ya udhibiti wa gugu maji.

### Huduma ya Ukaguzi wa Mazao

**93.** Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti uingizaji nchini wa visumbufu vya mimea na mazao, ukaguzi wa mazao yanayoingizwa nchini na yanayosafirishwa nje ya nchi uliendelezwa katika vituo vyote vya mipakani. Jumla ya tani 959,813 za mazao mbalimbali zilikaguliwa ambapo tani 327,917 zilikuwa za mazao yaliyosafirishwa nje ya nchi na tani 631,896 za mazao mbalimbali zilikaguliwa na kuruhusiwa kuingizwa nchini baada ya kuthibika kwamba hazina visumbufu. Jumla ya vyeti 4,645 vya usafi wa mazao vilitolewa kuthibitisha mazao hayakuwa na visumbufu hatari vya mimea. Baadhi ya mbegu zilizokaguliwa na kuingizwa nchini baada ya kuonekana hazina magonjwa na wadudu ni tumbaku, miwa, zabibu na muhogo.

## XI. MAFUNZO YA KILIMO KWA WATAALAM NA WAKULIMA

**94.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2002/2003, Wizara iliendelea kutoa mafunzo na kujenga uwezo wa taasisi na wataalam wake wa kutoa mafunzo yenye lengo la kuwawezesha wataalam na wakulima kuendesha kilimo cha kibiashara. Mfumo huu umesisitiza dhana ya elimu kwa vitendo kwa kuvitaka vyuo vilime mashamba makubwa ili kujenga fikra za kuendesha kilimo kikubwa cha kibiashara kwa wanachuo. Aidha, Wizara imerekebisha mitaala ya vyuo kwa kuingiza masomo ya kilimo cha kibiashara, hifadhi ya mazingira na elimu ya UKIMWI ili kuwapatia wahitimu elimu ya kujiajiri, kufundisha kilimo cha kibiashara na kuelimisha wakulima juu ya mbinu za kujikinga na maambukizi ya virusi vya UKIMWI. Mafunzo hayo yametolewa kama ifuatavyo:-

### Mafunzo kwa Wataalam Wapya na Maafisa Ugani

**95.** Vyuo vya Kilimo vilikuwa na wanafunzi 579, ikiwa ni ongezeko la asilimia 6 ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi 548 waliokuwepo vyuoni mwaka wa 2001/2002.

Aidha, Wizara ilitoa mafunzo ya rejea kwa maafisa ugani 140 wanaofundisha na kushauri wakulima juu ya kanuni bora za uzalishaji wa zao la pamba.

### Mafunzo kwa Wakulima

**96.** Katika mwaka wa 2002/2003, jumla ya wakulima 6,031 (wanawake 2,524 na wanaume 3,507) walipata mafunzo katika vyuo vya Kilimo vya Uyole, Ukiriguru, Mtwara, Ilonga, Igurusi, Mlingano, "*Kilimanjaro Agricultural Training Institute*" (KATC) Moshi na Chuo cha Taifa cha Sukari Kidatu, Kilombero. Hili ni ongezeko la asilimia 158 ikilinganishwa na mwaka wa 2001/2002 ambapo wakulima 3,803 walifundishwa. Ongezeko hili linatokana na Wizara kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya mafunzo kwa wakulima ambapo wakulima 3,044 waligharamiwa na Serikali. Halmashauri za Wilaya ziligharamia wakulima 810 na wahisani wakulima 2,177.

**97.** Mafunzo yaliyotolewa kwa wakulima yalihusu kilimo cha maksai, usindikaji wa mazao, kilimo cha miwa kwa wakulima wadogo, hifadhi ya mazingira na elimu ya UKIMWI. Jumla ya wakulima 1,079 wakiwemo wanawake 491 walihudhuria kozi za uzalishaji wa zao la mpunga kwa kutumia kilimo cha umwagiliaji maji mashambani katika chuo cha kilimo cha KATC, Moshi. Mafunzo hayo yaligharimiwa na Wizara (wakulima 1,009), Halmashauri za Wilaya na Manispaa (wakulima 55) na Vyuo vya Kilimo (wakulima 15).

### Mafunzo ya Wataalam wa Kilimo Nje ya Nchi

**98.** Katika kuimarisha taaluma mbalimbali, jumla ya watumishi 134 walipatiwa mafunzo ya muda mfupi na mrefu nchi za nje ambapo watumishi 16 walitoka Halmashauri za Wilaya na watumishi 118 walitoka Wizara ya Kilimo na Chakula. Mafunzo hayo yalifadhiliwa na Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa, Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo wa Kimataifa na Balozi za Denmark, Japan, Misri, Uholanzi, Ujerumani, Uingereza, Ireland, Australia, Sweden na Marekani.

### Urekebishaji wa Mitaala

**99.** Katika mwaka wa 2002/2003, Wizara imerekebisha mitaala mitano ya vyuo vya kilimo kwa kuingiza masomo ya kilimo cha biashara, kilimo cha maksai, usindikaji wa mazao, elimu ya UKIMWI na hifadhi ya mazingira ili kuwapatia wahitimu elimu itakayowawezesha kujiajiri na kufundisha kilimo cha biashara. Katika kutekeleza kilimo cha mashamba makubwa, vyuo vya kilimo vimelima mashamba yenye ukubwa wa ekari 1,100 kama ifuatavyo: Uyole (ekari 300), Mlingano (ekari 300), Ilonga (ekari 150), Ukiriguru (ekari 150), Naliendele (ekari 100) na Igurusi (ekari 100).

### Utayarishaji wa Vitabu

**100.** Katika mwaka wa 2002/2003, ili kukabiliana na upungufu wa vitabu vya kiada na rejea, jumla ya vitabu 13 vya fani za kilimo na mifugo vilitayarishwa. Vitabu hivyo vinahusu matumizi bora ya mali asili, kilimo cha biashara, utunzaji na uzalishaji wa ng'ombe wa maziwa, uzalishaji wa vipando vya mazao na afya ya wanyama. Vitabu vingine vilihusu, udhibiti wa magonjwa ya mimea na wadudu waharibifu wa mimea, matumizi bora ya maji kwa kilimo cha umwagiliaji maji mashambani, sifa za mbegu bora za mazao, uzalishaji wa ng'ombe wa nyama, ulishaji na malisho ya mifugo, uzalishaji wa kuku na nguruwe na matumizi ya wanyamakazi katika kilimo.

**101.** Wizara ilikamilisha uandaaji wa kitabu cha Kiongozi cha Mkufunzi wa Somo la Kilimo cha Kibiashara na kukisambaza katika vyuo vyote vya kilimo na kwa wadau, ili kitumike kama kiongozi cha mkufunzi wa somo hilo. Aidha, kazi ya kuhuisha muhtasari wa kufundishia somo la kilimo cha umwagiliaji maji mashambani ngazi ya stashahada ilikamilika.

## XII. UBINAFSISHAJI WA MASHIRIKA YA KILIMO

**102.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2002/2003, Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (PSRC) iliendelea na zoezi la ubinafsishaji wa mashamba na mali za mashirika ya umma chini ya Wizara ya Kilimo na Chakula. Chini ya mpango huo, Vinu vya Shirika la Usagishaji la Taifa (NMC) vya Mwanza, Shinyanga na Mzizima vilibinafsishwa. Aidha, Serikali iliamua kuwa baadhi ya mali za NMC zibaki serikalini kwa ajili ya Hifadhi ya Chakula ya Taifa. Mali hizo ni vinu, vihenge *(silos)* na maghala yaliyoko Kurasini, Dar es Salaam, Unga Limited katika Manispaa ya Arusha, Barabara ya Uhuru katika Manispaa ya Iringa, eneo la viwanda Dodoma na maghala ya Vwawa, Mbozi. Serikali imeamua kwamba kati ya maghala 28 ambayo hayajabinafsishwa, maghala 17 yatangazwe na kuuzwa moja moja na maghala 11 yauzwe kwa vyama vya ushirika vilivyoomba kuyanunua.

**103.** Uchambuzi wa hisa za kiwanda cha TANICA zitakazouziwa vyama vya Ushirika na zitakazouzwa kwenye soko la wazi umefanyika. Aidha, Jineri ya Bodi ya Pamba iliyoko Manawa ilifanyiwa uthamini tayari kwa kutangazwa kuuzwa. Hatima ya ubinafsishaji wa Kiwanda cha Lupembe na Shamba la Mlangali inasubiri uamuzi wa mahakama.

**104.** Mheshimiwa Spika, kuhusu ubinafsishaji wa mashamba ya NAFCO, Serikali iliamua mashamba ya Dakawa, Ruvu, Mbarali na Kapunga yabinafsishwe kwa wakulima wadogo. Shamba la Ruvu lenye hekta 720 limekarabatiwa na Wizara na limeanza uzalishaji wa mpunga. Wakulima 720 watauziwa shamba hilo na wameunda Chama cha Ushirika Ruvu Ltd. (CHAURU) kitakachowahudumia wakulima wa shamba hilo. PSRC wanaendelea na ubinafsishaji wa mali nyingine za shamba la Ruvu. Mashamba ya mpunga ya Dakawa, Mbarali na Kapunga yanafanyiwa uchambuzi wa kina na yataandaliwa utaratibu wa kuwauzia wakulima wadogo watakaoyamiliki. Aidha, mashamba ya ngano ya Hanang na viwanda 12 vya korosho viliendelea kutafutiwa wawekezaji.

## XIII. KUREKEBISHA NA KUHUISHA SHERIA

**105.** Mheshimiwa Spika, Sheria za Bodi za Sukari, Tumbaku, Kahawa na Pamba na kanuni zake zilirekebishwa katika mwaka wa 2002/2003. Vilevile, sheria ya Hakimiliki za Wazalishaji na Watafiti wa mbegu ilipitishwa na Bunge hili Tukufu tarehe 7 Novemba, 2002 kwa lengo la kulinda haki za wazalishaji wa aina mbalimbali za mbegu na kuwa kichocheo cha uzalishaji zaidi wa mbegu bora nchini. Muswada wa Sheria mpya ya mbegu umeandaliwa na unatarajiwa kuwasilishwa Bungeni mwezi wa Oktoba, 2003.

## XIV. HIFADHI NA USALAMA WA CHAKULA

**106.** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo na Chakula ina jukumu la kuhakikisha kwamba Taifa linakuwa na uhakika wa upatikanaji wa chakula wakati wote na kuwa wananchi wanapata lishe bora ya kuwawezesha kuishi maisha yenye afya na hivyo kutekeleza majukumu yao ya kiuchumi na kijamii. Ili kufikia lengo hilo, kazi kuu zilizofanywa katika mwaka wa 2002/2003 ni kama ifuatavyo:-

- Kununua na kuhifadhi nafaka katika Hifadhi ya Chakula ya Taifa kwa lengo la kukabiliana na matukio ya upungufu wa chakula punde yanapotokea.
- Kukusanya taarifa na takwimu za hali ya mvua na mazao mashambani, kufuatilia hali ya chakula na kusambaza taarifa kuhusu hali ya chakula.
- Kutoa huduma za kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno na usindikaji kwa kuibua teknolojia zilizopo, kuandaa vitabu na mpango wa kusambaza teknolojia hizo katika Halmashauri na kwa wakulima.
- Kuandaa Sera ya Usalama wa Chakula

### Hifadhi ya Chakula ya Taifa

**107.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2002/2003, Hifadhi ya Chakula ya Taifa ilinunua tani 28,475 za mahindi. Lengo lilikuwa kununua tani 20,900. Hii ilitokana na fedha zote zilizoombwa kutoka Hazina kwa ajili ya kununulia mahindi kupatikana katika wakati uliopangwa. Kiasi cha mahindi kilichonunuliwa kiliongeza akiba ya chakula iliyokuwepo ya tani 47,048 kufikia tani 75,523. Katika kipindi hiki, mauzo ya mahindi yalifanywa kwa Serikali ya Zambia, iliyouziwa jumla ya tani 4,839, Idara ya Magereza, Tani 6,879 na Mkoa wa Arusha tani 2,043. Hadi tarehe 16 Juni, 2003, akiba ya chakula katika Hifadhi ya Chakula ya Taifa ilikuwa tani 51,971. Akiba hiyo inahifadhiwa kwenye kanda 7 za Kipawa – Dar es Salaam (tani 5,121), Arusha (tani 19,210), Dodoma (tani 11,302), Shinyanga (tani 7,607), Makambako – Iringa (tani 4,696), Songea – Ruvuma (tani 3,209) na Sumbawanga – Rukwa (tani 822).

### Usalama wa Chakula

**108.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2002/2003 Wizara iliendelea na kazi ya kufuatilia hali ya mvua na mazao ya chakula mashambani. Tathmini ya Mwisho ya uzalishaji wa mazao ya chakula ilifanywa mwezi wa Agosti, 2002 na kuthibitisha kuwa Taifa lingejitosheleza kwa chakula kwa asilimia 102. Hata hivyo, mwanzoni mwa mwaka wa 2003, wakati hali ya ukame ilipojitokeza katika maeneo yote ya nchi, Wizara ilijiwekea utaratibu wa kufuatilia kwa karibu hali ya mvua na mazao mashambani kwa vipindi vya kila wiki. Mikoa na wilaya ilionyesha ushirikiano mkubwa wa kuwasilisha taarifa za hali ya chakula ambazo ziliiwezesha Serikali kujiandaa kukabiliana na hali ya upungufu wa chakula. Aidha, kazi nyingine zilizofanywa ni pamoja na kujenga mfumo wa kuhifadhi taarifa na takwimu za usalama wa chakula na uandaaji wa mtandao wa kusambaza taarifa na takwimu hizo kupitia tovuti na kuendesha mafunzo ya watakwimu kilimo wa mikoa na wilaya kutoka mikoa ya Mbeya na Rukwa.

### Udhibiti wa upotevu wa mazao ya chakula baada ya mavuno

**109.** Mheshimiwa Spika, hasara inayotokana na kuharibika kwa mazao baada ya mavuno bado ni kubwa na inaathiri kipato cha wakulima na upatikanaji na usalama wa chakula. Mheshimiwa Spika, Wizara imeimarisha uwezo wake wa kutoa huduma za kupunguza upotevu wa mazao ya chakula baada ya kuvuna, kwa kuandaa maandiko ya kuwafundisha wataalam na wakulima teknolojia za kuhifadhi na kusindika mazao ya chakula. Maandiko haya yanahusu mbinu bora za hifadhi, usindikaji na utunzaji wa mazao ya nafaka, mikunde, mboga na matunda, mazao ya mizizi, mazao ya mbegu za mafuta na mazao ya viungo.

**110.** Vitabu 6 vya mwongozo wa matumizi ya teknolojia hizo kwa mazao muhimu ya chakula hususan mazao ya nafaka, mikunde, mboga na matunda, mazao ya mizizi, mazao ya

mbegu za mafuta na mazao ya viungo vimetayarishwa pamoja na vitabu viwili vya mafunzo *(Training Manuals)* kwa maafisa ugani wa wilaya vimeandaliwa. Vitabu hivi vitasambazwa kwa maafisa ugani na wadau wengine. Aidha, jumla ya vipeperushi 6 viliandaliwa katika taaluma ya ujenzi wa ghala aina ya s*ilo*, utunzaji wa ghala na hifadhi, ujenzi wa kihenge bora, ujenzi wa kichanja bora (c*rib)* cha kukaushia mazao, kaushio bora la kutumia mionzi ya jua kwa ajili ya mboga na matunda na kichanja bora cha kukaushia nafaka. Vile vile, Wizara ilitoa msukumo mpya katika kupunguza upotevu wa mazao ya chakula kwa kukipatia jukumu la kuainisha teknolojia na kuandaa miongozo ya kusambaza teknolojia na elimu kuhusu matumizi bora ya vyakula.

**111.** Mheshimiwa Spika, usalama wa chakula ni suala la msingi kwa wananchi wote. Hata hivyo, sehemu kubwa ya wananchi hususan katika ngazi ya kaya hawajaweza kuwa na uhakika na usalama wa chakula. Uandaaji wa Sera ya Usalama wa Chakula ni hatua muhimu ambayo imekusudiwa kuweka mfumo endelevu wa kuratibu masuala yote yanayohusu usalama wa chakula ikiwa ni pamoja na kutoa mwelekeo na miongozo katika sera kuhusu: uzalishaji, upatikanaji, masoko na biashara ya mazao ya ndani na nje ya nchi, taarifa na takwimu za hali ya chakula, hatua za kuchukuliwa katika nyakati za njaa, hifadhi na usindikaji na matumizi ya chakula. Maandalizi ya Sera ya Usalama wa Chakula yalianza mwezi wa Januari, 2003. Rasimu ya awali ya Sera ilitazamiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2003, kabla ya kuwasilishwa Serikalini.

## XV. USINDIKAJI WA MAZAO

**112.** Mheshimiwa Spika, usindikaji wa mazao ni muhimu katika kuongeza thamani ya mazao, kipato kwa mkulima na kupanua wigo wa matumizi ya mazao. Katika mwaka 2002/2003, lengo la Wizara lilikuwa kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha na kuendeleza viwanda vya kusindika mazao ya kilimo ili kuongeza ubora wa mazao. Ili kufanikisha lengo hilo, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Viwanda na Biashara na Shirika la Maendeleo ya Viwanda la Umoja wa Mataifa (UNIDO), ilihamasisha sekta binafsi kuingiza nchini teknolojia za usindikaji wa mazao na kupanua matumizi ya teknolojia zilizopo nchini. Aidha, mkazo uliwekwa katika matumizi ya njia asili za usindikaji wa mazao na kushirikisha vikundi vya vijana na kinamama. Serikali iliendelea kuweka vivutio kwa wawekezaji kutoka nje na ndani kuwekeza katika kuanzisha au kufufua viwanda vya usindikaji wa mazao.

**113.** Uwekezaji katika viwanda vya kusindika mazao ya biashara hususan chai, kahawa, sukari, pamba na korosho umeonyesha mafanikio. Uwekezaji katika zao la sukari umeongeza uzalishaji wa sukari nchini kutoka tani 113,622 za sukari mwaka wa 1998 hadi kufikia tani 163,000 katika msimu wa 2001/2002 na tani 190,120 katika msimu wa 2002/2003. Viwanda vya kubangua korosho vya Masasi na Kibaha vilikarabatiwa na kukodishwa kwa wawekezaji. Viwanda hivi vina uwezo wa kubangua jumla ya tani 20,000. Aidha, kiwanda cha *Premier Cashew* na *Mohamed Enterprise* vimeendelea kubangua korosho kwa kutumia mashine ndogo za mikono. Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote umewasaidia wananchi wa Dar es Salaam, Pwani na Mtwara kwa kuwapatia mashine ndogo ndogo za kubangua korosho kwa mikono. Aidha, Mfuko umewapatia mafunzo na ajira wananchi 100 wa mkoa wa Mtwara kuhusu ubanguaji wa korosho. Utaratibu wa kutoa mafunzo kwa kituo cha Dar es Salaam utaanza msimu ujao. Kiwanda cha Nyumbu kimeagizwa kutengeneza mashine nyingi za kubangua korosho.

**Mfuko wa Pamoja wa Msaada wa Chakula Kati ya Tanzania na Japan (Tanzania – Japan Food Aid Counterpart Fund - FACF)**

**114.** Katika mwaka wa 2002/2003 jumla ya Shilingi bilioni 1.615 zilitolewa na Mfuko wa Pamoja wa Msaada wa Chakula Kati ya Japan na Tanzania (FACF) kugharamia miradi midogo ya maendeleo katika sekta ya kilimo. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 795 ziligharamia ukarabati wa skimu saba za kilimo cha umwagiliaji maji mashambani. Skimu zilizonufaika na msaada huo ni Ghona, hekta 450, iliyoko Moshi Vijijini; Yavayava, hekta 100 iliyoko Mkuranga; Kirya, hekta 350, iliyoko Mwanga; Segeni hekta 100, iliyoko Rufiji; Kitivo, hekta 450, iliyoko Lushoto na Mloa Malinzanga, hekta 400 iliyoko Iringa Vijijini.

## XVI. MAENDELEO YA WATUMISHI

**115.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2002/2003, zoezi la kupandisha vyeo watumishi wa Wizara liliendelea. Jumla ya watumishi 1,858 walipandishwa vyeo na mamlaka husika wakiwemo watumishi 328 ngazi ya KAMUS, watumishi 1,176 ngazi ya Tume Ajiri na watumishi 354 ngazi ya Rais. Zoezi bado linaendelea.

## XVII. MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA 2002/2003FEDHA ZILIZOIDHINISHWA NA KUTOLEWA

**116.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2002/2003, Wizara ya Kilimo na Chakula ilitengewa shilingi bilioni 34.3 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 15.7 zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 18.6 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo, shilingi bilioni 1.8 zilikuwa ni fedha za hapa na shilingi bilioni 16.8 zilikuwa fedha za kigeni.

### Bajeti ya Matumizi ya Kawaida

**117.** Wizara ya Kilimo na Chakula ilitengewa shilingi bilioni 15.7 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi tarehe 20 Juni 2003 Wizara ilikuwa imekwishapokea jumla ya shilingi bilioni 15.03 sawa na asilimia 96 ya kiasi kilichoidhinishwa. Hadi tarehe 20 Juni, 2003, kiasi cha fedha kilichokuwa kimetumika kilikuwa shilingi bilioni 14.25 sawa na asilimia 95 ya kiasi kilichopokelewa na asilimia 91 ya kiasi kilichoidhinishwa.

### Bajeti ya Matumizi ya Maendeleo

**118.** Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa 2002/2003, Wizara ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 18.6 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 1.8 ni fedha za hapa na shilingi bilioni 16.8 ni fedha za kigeni. Hadi tarehe 20 Juni 2003 kiasi cha shilingi bilioni 1.8 fedha za hapa zilitolewa na kutumiwa na miradi. Kiasi hicho ni sawa na asilimia mia moja ya fedha iliyoidhinishwa. Hadi kufikia tarehe 20 Juni, 2003 miradi ilikuwa imetumia shilingi bilion 13.4 ya fedha za nje. Matumizi haya ni sawa na asilimia 80 ya fedha za nje zilizotengwa. Matumizi haya madogo yanatokana na muda mrefu unaotumika kuagiza vifaa na magari kwa ajili ya matumizi ya miradi. Sababu nyingine ni utaratibu mrefu uliopo wa kuwapata makandarasi kwa njia za zabuni na uwezo mdogo wa baadhi ya makandarasi wa ndani kukamilisha ujenzi ndani ya muda wa makubaliano.

## XVIII. KAZI ZITAKAZOFANYIKA NA MATARAJIO KATIKA MWAKA WA 2003/2004

**119.** Mheshimiwa Spika, mwaka wa 2003/2004 ni mwaka wa pili wa utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo. Katika mwaka wa 2003/2004, Wizara itaendelea kuelekeza uwekezaji katika mambo yenye manufaa ya moja kwa moja kwa mkulima na yatakayotoa matokeo yaliyotarajiwa katika muda mfupi *(quick wins)* kutokana na kuwepo kwa tishio la ukame na pengine hata njaa katika mwaka wa 2004. Wizara itaelekeza juhudi zake kuuandaa umma ili utekeleze mikakati ya kukabiliana na hali hiyo.

**120.** Kumbukumbu zilizopo za historia ya nchi yetu zinaonyesha kwamba, mwaka wa 1874 na kila mwaka unaoishia na namba 4, yaani kila baada ya mzunguko wa miaka 10, nchi yetu hukabiliwa na ukame. Katika miaka ya karibuni, wazee wetu wanakumbuka njaa kali au upungufu wa chakula uliotokea katika miaka ya 1944, 1954 na 1964. Aidha, wengi wetu tunakumbuka sababu zilizopelekea kuanzishwa kwa kampeni za Siasa ni Kilimo na Kilimo cha Kufa na Kupona katika miaka ya 1970 na 1980. Kampeni hizo, zilitokana na ukame uliotokea miaka wa 1974 na 1984. Kwa kuwa taifa letu lilikabiliwa tena na hali ya ukame mwaka wa 1994, kuna uwezekano mkubwa kwamba, mwaka wa 2004, Taifa litakabiliwa tena na ukame ambao utasababisha upungufu wa chakula na pengine njaa.

**121.** Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2002/2003, tayari hali ya ukame imejitokeza na imeathiri uzalishaji wa mazao ya chakula na ya biashara katika baadhi ya maeneo hayo na kusababisha upungufu wa chakula katika maeneo ya nchi na kuathiri uzalishaji wa mazao makuu ya biashara, hususan zao la pamba. Kutokana na hali hiyo ya ukame na tishio la upungufu wa chakula, Wizara, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004 imepanga kuelekeza juhudi zake katika kuhimiza wakulima kuongeza tija na uzalishaji wa mazao yanayostahimili ukame, hususan zao la muhogo.

**122.** Mheshimiwa Spika, kutokana na tathmini iliyofanywa na Wizara kuhusu hali ya chakula na kumbukumbu zilizopo zinaonyesha kwamba maeneo yote yanayolima muhogo hayana upungufu wa chakula. Mfano mzuri ni Wilaya za Mkoa wa Mara, hususan Serengeti na Bunda ambazo zina akiba ya muhogo mashambani wanaoweza kuutumia kwa muda wa miaka miwili mfululizo. Haya ni mafanikio makubwa na yanafaa kuigwa, kuenezwa nchi nzima na kupongezwa.

**123.** Mheshimiwa Spika, suala la upungufu wa chakula sio jambo la kuchezea na kwa kuwa jawabu endelevu la kupambana na hali hiyo lipo katika kilimo cha zao la muhogo na mazao mengine yanayostahimili ukame, kilimo cha mazao hayo kinapaswa kisiwe jambo la hiari. Viongozi wote wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, Wakuu wa Mikoa, Wilaya hadi Vijiji, tunapaswa kutekeleza maagizo ya Rais ya tarehe 31 Machi, 2003, kwa kupanda zao la muhogo popote linapositawi.

**124.** Katika mwaka wa 2003/2004, ili kukabiliana na hali ya ukame na upungufu wa chakula unaoweza kujitokeza, Wizara imepanga kutekeleza mambo yafuatayo:-

- **Kuhimiza kilimo cha mazao yanayostahimili ukame:** Ili kuhakikisha Taifa lina uwezo wa kukabiliana na upungufu wa chakula unaosababishwa na hali ya ukame, Wizara itahimiza kilimo cha mazao yanayostahili ukame hususan muhogo, mtama, uwele, mikunde na viazi vitamu.

- **Kutia mkazo kilimo cha umwagiliaji maji mashambani:** Wizara itahakikisha skimu zote za umwagiliaji maji mashambani zina mifumo ya usimamizi utakaohakikisha kwamba zinatumika kikamilifu kuzalisha mazao ya chakula. Aidha, Wizara itaendelea kukarabati skimu za zamani na kujenga skimu mpya kwa mujibu wa Mpango Kabambe wa Umwagiliaji Maji Mashambani.
- **Kudhibiti magonjwa na visumbufu vya mimea na mazao:** Wizara itaendelea kuimarisha uwezo wake wa kudhibiti kikamilifu milipuko ya visumbufu vya mimea na mazao, hususan kwelea kwelea, panya, viwavijeshi na nzige.
- **Kuhifadhi udongo na kusimamia matumizi bora ya ardhi:** Ili kudhibiti uharibifu wa ardhi unaotokana na mmomonyoko wa udongo na kuongeza upatikanaji wa maji kwa mazao yaliyopo mashambani, Wizara itahimiza kilimo cha matuta na makinga-maji.
- **Hifadhi ya Chakula ya Taifa:** Hifadhi ya Chakula ya Taifa itanunua tani 20,799 za mahindi. Kiasi hiki kikijumuishwa na akiba iliyopo ya tani 51,971 kitaongeza akiba ya mahindi ifikie tani 72,720. Ununuzi wa akiba utafanywa kwenye maeneo yenye ziada na kuuzwa kwa wananchi kwenye maeneo yenye upungufu wa chakula.
- **Kusambaza teknolojia za kudhibiti upotevu wa mazao baada ya mavuno:** Ili kuhakikisha kuwa chakula kinachovunwa kinahifadhiwa katika hali ya usalama na kupunguza uwezekano wa kuharibika kutokana na mashambulizi ya wadudu, Wizara itahakikisha viuatilifu bora vya udhibiti vinapatikana na wakulima watahimizwa kutumia mbinu za kupambana na visumbufu vya mazao baada ya mavuno.

**125.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004 zaidi ya kupambana na hali ya ukame, Wizara itatekeleza kazi zifuatavyo:-

- **Kupanua wigo wa mikopo inayotolewa na Mfuko wa Pembejeo za Kilimo**: Mfuko wa Pembejeo utaendelea kutoa mikopo kwa ajili ya uagizaji na usambazaji wa pembejeo na zana za kilimo kwa kupitia benki na utatoa mikopo kununulia matrekta mapya na kukarabati ya zamani. Shilingi bilioni 3.6 zimetengwa kwa ajili ya Mfuko.
- **Kuhimiza kilimo cha mazao yasiyo asili:** Wizara itahimiza uzalishaji wa mazao yasiyo asili kwa lengo la kumwezesha mkulima kupata mazao yenye bei nzuri na uhakika katika soko la ndani na nje ya nchi. Mazao hayo ni pamoja na paprika, vanilla na pilipili manga na migomba bora.
- **Kuendeleza matumizi ya zana bora za kilimo:** Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za wilaya itafufua vituo vya wanyamakazi na kuwafundisha wakulima matumizi ya zana bora za kilimo. Wizara itahamasisha sekta binafsi kuagiza matrekta mapya na yaliyotumika. Aidha, sekta binafsi itahamasishwa kuanzisha na kuendesha vituo vya matrekta kibiashara.
- **Kuimarisha huduma za utafiti wa mazao:** Huduma za utafiti zitaimarishwa kwa kuhakikisha vituo vya utafiti vinapata huduma muhimu za umeme, maji na mawasiliano kwa uhakika zaidi ili viweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.
- **Kuongeza uzalishaji wa mbegu za mazao ya kilimo:** Lengo ni kuzalisha tani 1,500 za mbegu za mahindi, mpunga na mikunde katika mashamba ya mbegu ya Arusha, Msimba, Dabaga Kilangali, Mwele na Vituo vya Utafiti.
- **Kueneza matumizi ya mbinu shirikishi na shamba darasa:** Mkazo utawekwa katika kuhamasisha viongozi Wakuu wa Mikoa na Viongozi wa Serikali za Mitaa,

kuhusu dhana ya Mbinu Shirikishi Jamii ili waielewe na wasimamie utekelezaji wake. Timu za wawezeshaji 100 za Wilaya, 2,000 za Kata na 6,000 za vijiji zitaundwa na kuimarishwa ili zichangie katika kueneza mbinu shirikishi jamii. Ili kuongeza kasi ya kueneza mbinu hizo na kuongeza ufanisi katika matumizi ya rasilimali, kazi hii itafanyika kwa ushirikiano na Wizara za Maji na Maendeleo ya Mifugo, Ushirika na Masoko, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wizara ya Kilimo na Chakula.

- **Kukamilisha maandalizi ya Sera ya Usalama wa Chakula na Kuandaa Mwongozo wa Utekelezaji wa Sera:** Mwongozo wa utekelezaji wa sera ya usalama wa chakula utaandaliwa. Aidha, Wizara itaandaa mapendekezo ya kurekebisha Sheria ya Usalama wa Chakula ya mwaka wa 1991.
- **Kukusanya takwimu za mvua na hali ya chakula:** Wizara itaimarisha uratibu na ukusanyaji wa taarifa na takwimu za mvua na hali ya mazao na upatikanaji wa chakula nchini.

**126.** **Mheshimiwa Spika,** Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo ambao uliandaliwa kwa pamoja na Wizara za Maji na Maendeleo ya Mifugo, Ushirika na Masoko, Kilimo na Chakula na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za mitaa unalenga kukuza kilimo na kuongeza uhakika na upatikaji wa chakula katika ngazi zote ili kuinua hali ya maisha ya wananchi hususan vijijini.

**127.** Aidha, Mkakati kwa kiwango kikubwa, utatekelezwa katika ngazi ya Halmashauri za Wilaya kupitia mipango yao ya kilimo ambayo imeandaliwa kwa *mbinu shirikishi jamii.* Wizara za Sekta ya Kilimo kwa pamoja na Halmashauri zimeandaa na kusambaza mwongozo wa kuwezesha Halmashauri za Wilaya kuandaa mipango yao ya kilimo. Baadhi ya mipango hiyo itaanza kutekelezwa mwaka wa 2003/2004.

**128.** Mipango ya Wilaya itakayoanza kutekelezwa kwa kutumia fedha za serikali inamlenga mkulima na mfugaji moja kwa moja na inalenga maeneo yanayotarajiwa kuleta matokeo ya haraka. Maeneo hayo ni ujenzi na ukarabati wa skimu ndogo za umwagiliaji maji mashambani kukarabati/kujenga malambo, majosho kwa ajili ya kuimarisha afya ya mifugo, kukarabati na kununua mashine za kupukuchua kahawa na kuimarisha baadhi ya Vyama vya Kuweka na Kukopa (SACCOs). Wizara za Sekta ya Kilimo kwa kushirikiana na Halmashauri zitaweka mfumo wa kusimamia kikamilifu mipango hiyo.

## XIX. MAZAO YA BIASHARA

**129.** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo na Chakula, itaendelea kusimamia na kuendeleza mazao makuu ya biashara hususan pamba, tumbaku, pareto, kahawa, korosho, miwa, mkonge na chai. Kutokana na ushindani mkubwa katika soko la dunia mazao yenye ubora wa chini hupata bei ya chini kabisa isiyoleta manufaa kwa wafanyabiashara na wakulima. Ili mkulima anufaike, ni muhimu azalishe mazao yenye ubora ambayo yatampatia bei kubwa katika soko.

**130.** Katika msimu huu wa 2003/2004, Wizara itasimamia ubora wa mazao yanayozalishwa nchini ili yawe na ubora wa hali ya juu na yatakayoweza kuuzwa kwa bei nzuri katika soko la ndani na nje. Mambo muhimu yatakayozingatiwa ni kuelimisha wakulima umuhimu wa kutunza mazao vizuri mashambani na kuyapanga katika madaraja wakati wa kuuza, kuimarisha huduma za ukaguzi wa mazao, kuhakikisha mazao yanauzwa katika vituo vilivyoidhinishwa na kuhimiza usindikaji wa mazao kabla ya kuuza.

Mategemeo ya uzalishaji wa mazao makuu ya biashara katika msimu wa 2003/2004 ni kama ifuatavyo:-

## Sukari

**131.** Uzalishaji wa sukari unatarajiwa kuongezeka kwa asilimia 30.4 kutoka tani 190,120 mwaka wa 2002/2003 hadi tani 248,000 mwaka wa 2003/2004. Ongezeko hili litatokana na uwekezaji zaidi katika viwanda vya Mtibwa na TPC Ltd na Kiwanda na mashamba ya Kampuni ya Sukari ya Kagera baada ya ubinafsishaji. Hali ya uzalishaji katika viwanda vya sukari inatarajiwa kuwa kama ifuatavyo:-

***Jedwali Na: 3 Uzalishaji wa Sukari 2002/2003 – 2003/2004***

| KIWANDA | 2002/2003 | 2003/2004 | Asilimia ya Ongezeko |
|---|---|---|---|
| Kilombero | 98,420 | 106,000 | 7.70 |
| Mtibwa | 36,850 | 50,000 | 35.70 |
| TPC Ltd. | 54,850 | 62,000 | 13.00 |
| Kagera | | 30,000 | - |
| **Jumla** | **190,120** | **248,000** | **30.40** |

***Chanzo*** *: Wizara ya Kilimo na Chakula na Bodi za Mazao*

**132.** Wizara, kwa kupitia Bodi ya Sukari, itasimamia na kuhakikisha kuwa wakulima wadogo wa mashamba ya miwa ya Kilombero, Mtibwa na Kagera wanapatiwa nyenzo muhimu za uzalishaji. Aidha, Wizara itahimiza mwekezaji kufufua mashamba ya Kiwanda cha Sukari cha Kagera na kuchangia katika kuanzisha kilimo cha wakulima wadogo wa miwa.

## Chai

**133.** Uzalishaji wa chai unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 28,028 mwaka wa 2002/2003 hadi tani 31,000 mwaka wa 2003/2004 sawa na ongezeko la asilimia 11. Ongezeko hilo litatokana na kuimarisha huduma za ugani, masoko na mikopo ya pembejeo kwa wakulima na ukarabati wa mashamba ya wakulima wadogo. Uzoefu uliopatikana katika mashamba ya Mwakaleli na Katumba wilayani Tukuyu, unaonyesha kwamba wakulima wakubwa na wenye viwanda vya chai wanaweza kusaidia wakulima wadogo kwa kuwapatia masoko ya uhakika kwa chai yao, kuwakopesha pembejeo za kilimo na kuwapa ushauri wa kilimo bora cha chai.

**134.** Hata hivyo juhudi za kuendeleza zao la chai zinakabiliwa na tatizo la baadhi ya wawekezaji kutozingatia wajibu wa kuendeleza viwanda na ukarabati au upanuaji wa mashamba ya chai waliyomilikishwa. Hali hii imejitokeza katika Kiwanda cha Lupembe (wilayani Njombe), Kiwanda na mashamba ya Maruku, na Shamba la Chai la Dabaga. Wizara inaendelea kufuatilia wawekezaji wa mashamba na viwanda vya kusindika chai. Ili kuongeza uzalishaji katika mashamba ya wakulima wadogo, wizara itaendelea kuwashawishi wenye mashamba makubwa na viwanda vya kusindika chai, kuwapatia wakulima wadogo huduma za pembejeo ili kuongeza tija na uzalishaji.

## Tumbaku

**135.** Uzalishaji wa tumbaku unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 31,700 mwaka wa 2002/2003 hadi tani 34,230 mwaka wa 2003/2004 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia nane. Ongezeko hilo litatokana na mafunzo ya kilimo bora cha tumbaku kwa wakulima.

Wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa wataalam na wakulima juu ya kilimo bora cha tumbaku ili kukabiliana na matatizo ya uzalishaji na upatikanaji wa soko. Wizara pia kwa kupitia Bodi ya Tumbaku, itafuatilia kwa karibu soko la tumbaku ili kupunguza udanganyifu wa bei kwa wakulima. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ushirika na Masoko, itahakikisha migongano kati ya wanunuzi wa tumbaku na wakulima, kwa mfano mgogoro uliopo hivi sasa kati ya wakulima wa tumbaku wa mkoa wa Iringa na wanunuzi wa zao la tumbaku unamalizwa.

## Kahawa

**136.** Uzalishaji wa zao la kahawa unatarajiwa kupungua kutoka tani 52,439 mwaka wa 2002/2003, hadi kufikia tani 51,000 mwaka wa 2003/2004 sawa na upungufu wa asilimia 0.83. Upungufu huo utatokana na tabia ya zao la kahawa kuzaa kwa wingi msimu mmoja na kupunguza uzalishaji katika msimu unaofuata. Msimu wa 2003/2004 unaangukia wakati kahawa inapunguza uzalishaji. Ili kuhakikisha mapato ya wakulima hayapungui, Wizara itaimarisha huduma za ugani ili kutoa elimu kwa wakulima juu ya uzalishaji wa kahawa yenye ubora wa juu. Ili kufanikisha lengo hili, juhudi kubwa itaelekezwa katika kufufua viwanda vya kupukuchua kahawa (*Central pulparies).* Juhudi zitaelekezwa katika kufufua ushirika hususan vyama vya msingi na kusisitiza usimamizi ili kuepusha upotevu wa fedha na rasilimali za wanachama.

**137.** Katika kukabiliana na magonjwa sugu ya kahawa kama vile chulebuni na kutu ya majani, Wizara itaendeleza mashamba ya miti mizazi yaliyoko Mbozi, Mbinga, Rombo, Hai na Arumeru kwa lengo la kuzalisha vikonyo vya kutosha vya aina za kahawa zinazostahimili magonjwa na kuvisambaza kwa wakulima. Utaratibu wa sasa wa mfumo wa upatikanaji wa pembejeo kwa njia ya vocha na Stakabadhi ya maghala (*Warehouse Receipt system*) utaimarishwa.

## Pareto

**138.** Uzalishaji wa pareto unatarajiwa kuongezeka kwa asilimia 17 kutoka tani 3,000 kwa mwaka wa 2002/2003 hadi tani 3,500 kwa mwaka wa 2003/2004. Mikakati ya kufikia lengo hili, ni pamoja na kusajili wanunuzi zaidi wa pareto ambao ni CARITAS Njombe, *Pyrethrum Processors and Growers (T) Ltd* na Kampuni ya H Range ambayo mbali na kununua pareto watawekeza katika shamba la Ibaga lililoko katika Wilaya ya Makete. Wizara, itaendeleza uzalishaji wa miche bora ya pareto yenye uwezo wa kuzalisha kilo 800 hadi 1000 za maua ya pareto kwa hekta na yenye viwango vya sumu vya asilimia 1.5 hadi 2.0 za sumu ikilinganishwa na aina inayozalishwa hivi sasa, inayozaa kilo 250 za maua kwa hekta na yenye asilimia 0.8 hadi 1.1 za sumu. Katika mwaka wa 2003/2004, Serikali kwa kupitia Wizara ya Ushirika na Masoko itatoa fedha kwa ajili ya kulipatia ufumbuzi tatizo la soko la zao la pareto kwa kununua pareto yote iliyo mikononi mwa wakulima.

## Korosho

**139.** Uzalishaji wa korosho unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 90,000 mwaka wa 2002/2003 hadi tani 125,000 mwaka wa 2003/2004, sawa na ongezeko la asilimia 38. Ili kufikia lengo hili, mkazo utawekwa katika kuhimiza matumizi ya kanuni bora za kilimo cha korosho, hususan kupalilia na kunyunyuzia dawa mikorosho dhidi ya ugonjwa wa *ubwiri unga* kwa wakati unaotakiwa. Aidha, Wizara kupitia Bodi ya Korosho itafuatilia kwa karibu soko la korosho ili kupunguza udanganyifu wa bei kwa wakulima.

## Pamba

**140.** Katika mwaka wa 2003/2004, uzalishaji wa zao la pamba unatarajiwa kupungua kutoka tani 188,690 za mwaka wa 2002/2003 na kufikia tani 162,000, ikiwa ni pungufu kwa asilimia 14.0. Upungufu huo umetokana na hali ya ukame inayoyakabili maeneo mengi yanayozalisha zao hili.

**141.** Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2003/2004, Wizara itahakikisha kwamba tatizo la uchanganyaji wa mbegu litakuwa limepatiwa ufumbuzi wa kudumu. Ili kufanikisha lengo hili, mbegu aina ya UK91 pekee ndiyo itakayokuwa inapandwa katika Ukanda wa Magharibi. Jumla ya tani 10,000 za mbegu hiyo zitasambazwa katika ukanda wa magharibi. Mbegu aina ya ALAI 90 pekee ndiyo itakayopandwa katika Ukanda wa Mashariki. Jumla ya tani, 250 za mbegu hiyo zitasambazwa katika maeneo hayo katika msimu wa 2003/2004. Mbegu hizi zina nyuzi ndefu na imara na zinavumilia ugonjwa wa mnyauko wa pamba na zinazaa pamba nyingi kuliko mbegu zilizopo.

**142.** Mheshimiwa Spika, mbegu zilizoondolewa masalia ya nyuzi kwa kutumia mashine zitaendelea kutumika chini ya usimamizi wa Bodi ya Pamba. Mbegu zilizoondolewa nyuzi kwa kutumia tindikali hazitatumika. Wizara kupitia Bodi ya Pamba na Taasisi ya Kusimamia Ubora wa Mbegu *(Tanzania Oficial Seed Certification Agency)* zitahakikisha kwamba mbegu zote zitakazotumika nchini zina sifa zote za mbegu bora na zina uwezo wa kuota na kuzalisha pamba bora. Matumizi ya mbegu hizo, yataenda sambamba na uchunguzi utakaofanywa juu ya matumizi ya mbegu zilizoondolewa masalia, kushauri juu ya uhifadhi wa mbegu hizo na mbinu bora za kuzipanda ili kupata uoto mzuri.

**143.** Ili kuhakikisha kuwa pamba inayozalishwa nchini ni ya ubora wa juu, Bodi ya Pamba itaendelea kuhakiki ubora wa pamba inayouzwa ndani na nje ya nchi kwa kutumia mtambo wa kisasa *(High Volume Instrument - HVI Spectrum II)* ambao utaanza kutumika mwaka wa 2003/2004. Mtambo huo umenunuliwa kwa kupitia mradi wa *Improvement of Cotton and Coffee Marketing and Trade* unaofadhiliwa na Mfuko unaojulikana kama '*Common Fund for Commodities'*.

**144.** Katika mwaka wa 2003/2004, viwanda vya kuchambulia pamba vilivyoko Moshi, na Kiberege (Kilombero) vitakarabatiwa, hatua ambayo itaongeza uwezo wa kuchambua pamba Kanda ya Pamba ya Mashariki kutoka tani 32,000 za sasa hadi tani 48,000 kwa mwaka. Teknolojia rahisi katika kilimo cha pamba, hususan zile za udhibiti wa wadudu wa pamba, zitaendelea kuenezwa kwa wakulima. Kutokana na maendeleo ya haraka ya teknolojia za udhibiti wa visumbufu vya zao la pamba, Wizara itahakikisha kuwa wakulima wanapata maelekezo ya kutosha ya matumizi ya teknolojia hizo, hususan matumizi ya mabomba mapya na viuatilifu vipya. Ili kuhakikisha upatikanaji na usambazaji wa pembejeo kwa wakati, Mfuko wa Kuendeleza Zao la Pamba utaeneza utaratibu wa kuandikisha wakulima na kuwapatia pembejeo kufuatana na kiwango cha pamba waliyozalisha.

**145.** Mheshimiwa Spika, mwaka wa 1999, Serikali ilizuia kilimo cha pamba katika mikoa ya kusini ili kudhibiti kuenea kwa funza mwekundu wa pamba katika maeneo mengine nchini. Ili kutafakari zaidi suala hili, tarehe 7 Juni 2003 Wizara iliandaa warsha iliyohudhuriwa na Waheshimiwa Wabunge wanaotoka katika maeneo yanayozalisha pamba na wataalam wa zao la pamba. Warsha ilipendekeza kuendelea kuwepo kwa karantini ya funza mwekundu nchini. Aidha, wajumbe wa warsha hiyo kwa pamoja walitoa changamoto

kwa watafiti kuendelea kutafuta mbinu mbadala ya kumdhibiti mdudu huyo. Wizara itashirikiana na taasisi za utafiti za kimataifa kutafuta mbinu za kumdhibiti mdudu huyo.

### Mkonge

**146.** Uzalishaji wa mkonge katika mwaka wa 2003/2004, unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 23,641 zilizozalishwa mwaka wa 2002/2003 hadi tani 25,000, sawa na ongezeko la asilimia 5.7 ikilinganishwa na uzalishaji wa mwaka wa 2002/2003. Ongezeko hili linatokana na upandaji uliofanyika toka mwaka wa 1999-2001 ambayo ni hekta 12,3000 ambazo zitavunwa mwaka wa 2003/2004. Ongezeko lingine ni kutokana na mkonge toka Kanda ya Ziwa (Mwanza, Mara na Shinyanga) ambayo itachangia karibu tani 3,500. Ili kuhakikisha kuwa sekta ya mkonge inakua, mkakati wa kuwahusisha wakulima wadogo katika Kilimo cha mkonge katika mikoa ya Mwanza, Mara na Shinyanga utaendelea kutekelezwa. Aidha Serikali kwa kushirikiana na Tume ya Rais ya kurekebisha Mashirika ya Umma itaendelea kufuatilia uendelezaji wa mashamba makubwa ya mkonge yaliyobinafsishwa kwa lengo la kubaini mashamba ambayo hayaendelezwi ili hatimaye yaweze kupatiwa wawekezaji wapya ambao watayaendeleza. Utafiti juu ya matumizi mengine ya mkonge kama gesi, karatasi, madawa na vifaa vya ujenzi utaendelezwa kwa kushirikiana na mashirika ya kimataifa kama UNIDO, *Common Fund for Commodities* chini ya uratibu wa kituo cha utafiti cha Mlingano na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

## XX. MAZAO YASIYO ASILI

**147.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004, Wizara itaendelea kuimarisha bustani za Serikali zilizoko Mpiji (Bagamoyo) na Songa (Muheza), Jaegetal na Malindi (Lushoto) kwa kuweka miundo mbinu ya umwagiliaji ili kuongeza ufanisi katika utunzaji wa vipando vya mazao yasiyo asili, hususan miti ya matunda na viungo. Aidha, bustani hizo zitatumika kutoa mafunzo kwa wataalam na wakulima juu ya kilimo bora cha mazao yasiyo asili. Kwa upande wa zao la ndizi, Wizara itaendelea kushirikiana na Halmashauri za Wilaya katika kuviwezesha vikundi vya wakulima kuanzisha mashamba kuzalisha miche ya migomba bora katika Wilaya za Morogoro, Mvomero, Ulanga, Kisarawe, Kibaha na Mkuranga.

### Uzalishaji wa Vanilla

**148.** Tathmini iliyofanyika mkoani Kagera inaonyesha kwamba wastani wa uzalishaji wa vanilla ni kilo 2,400 kwa hekta na wastani wa bei anayopata mkulima ni shilingi 8,000 kwa kilo ya vanilla mbichi. Kutokana na mafanikio hayo, mwaka wa 2003/2004 Wizara itaendelea kuhimiza kilimo cha vanilla katika mkoa wa Kagera. Aidha, itaanzisha majaribio ya uzalishaji wa zao hilo katika mashamba ya wakulima mkoani Morogoro.

### Uzalishaji wa Paprika

**149.** Zao la paprika ni mojawapo ya mazao yasiyo asili yanayopata umaarufu mkubwa na hivi sasa linazalishwa katika wilaya za Iringa vijijini, Iringa Mjini, Njombe, Kilosa, Kilombero, Songea Vijijini, Songea Mjini, Namtumbo, Mbeya Vijijini, Ileje, Arumeru, Same na Mwanga. Katika msimu wa 2003/2004 Wizara itaendelea kuhimiza wafanyabiashara kuingia mikataba ya uzalishaji na wakulima wa zao la paprika katika maeneo ambayo zao hilo linasitawi vizuri, hususan katika mikoa ya Arusha, Iringa, Kilimanjaro, Mbeya na Ruvuma.

### Uzalishaji wa Pilipili Manga

**150.** Zao la pilipili manga linazalishwa katika wilaya za Muheza, Lushoto, Same, Morogoro Vijijini na Mvomero. Humu nchini bei ya zao hili ni shilingi 1,000 hadi 1,500 na shilingi 1,500 na 5,500 kwa kilo moja katika soko la dunia. Katika mwaka wa 2003/3004 Wizara itaendelea kulifanyia tathmini zao hili katika Kituo cha Utafiti cha KATRIN, Morogoro na katika mashamba ya wakulima ili kubaini aina zenye nasaba bora na zinayozaa kwa wingi.

### Kilimo cha Migomba Bora (Migomba ya Biashara)

**151.** Zao hili linazalishwa kwa wingi katika mikoa ya Kagera, Kilimanjaro, Kigoma, Mbeya na Morogoro. Aina nyingi za migomba inayolimwa nchini ni ya asili ambayo ina tija ndogo ikilinganishwa na migomba bora. Migomba ya asili huzalisha tani 5.5 hadi 7 tu za ndizi kwa hekta ikilinganishwa na tani 20 hadi 60 kwa hekta kwa kutumia migomba bora. Migomba bora ambayo tayari imeingizwa nchini ni ya aina za *Embeailuma, Williams, Granaine, Gold Finger* na *Pazi*. Ili kuhakikisha kuwa miche ya kutosha ya migomba hiyo inapatikana kwa wingi na haraka, Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kutumia Kituo cha Utafiti wa Mazao ya Mboga na Matunda HORTI, Tengeru na Kituo cha Mpiji, Pwani itazalisha miche ya migomba bora na kuisambaza katika Mikoa ya Morogoro, Pwani na Dar es Salaam.

## XXI. HUDUMA ZA UTAFITI WA KILIMO

**152.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004, msukumo wa utafiti utaendelea kuhakikisha upatikanaji wa teknolojia bora za kilimo kwa wakulima. Juhudi za kuzalisha kwa wingi mbegu za mazao zitaendelezwa pamoja na uchunguzi wa aina bora zaidi za mbegu zitakazoweza kumpatia mkulima mavuno mengi na kuongeza tija katika mazingira mbalimbali ya uzalishaji. Wizara itaendelea kutathmini mazao mapya ya viungo na yasiyo ya asili kwa lengo la kuongeza wigo wa mazao ya biashara. Aidha, utafiti huu utafanyika kwa kulenga mahitaji halisi ya wakulima na utawashirikisha, kupitia mbinu shirikishi jamii, kuainisha matatizo yaliyopo na jinsi ya kuyatatua. Sehemu kubwa ya majaribio ya utafiti yatafanyika katika mashamba ya wakulima ili waweze kuhusika katika kuchagua teknolojia wanazozitaka.

**153.** Mheshimiwa Spika, vituo vya utafiti vitaendeleza tathmini ya aina za mbegu zinazostahimili ukame, magonjwa na wadudu waharibifu na zenye kutoa mavuno mengi kama ifuatavyo:

**154.** **Kituo cha Selian (Arusha)**, kwa kushirikiana na shamba la mbegu la Arusha kitaendelea kuzalisha na kuboresha mbegu mama (*Breeder seeds*) na za msingi za mahindi aina ya *Situka* na *Lishe* na ngano aina ya *Chiriku*.

**155.** **Kituo cha Uyole (Mbeya)**, kitazalisha na kuboresha mbegu chotara ya mahindi aina ya UH615 ambayo hustahimili ugonjwa wa ukungu wa majani (*Grey Leaf Spot*). Kituo pia kitazalisha mbegu za mazao ya maharage na soya ili kuwauzia wakulima. Aidha, kituo kitaendeleza uzalishaji *(multiplication)* wa mbegu mpya za pareto.

**156.** **Kituo cha Ukiriguru (Mwanza)**, kitaendelea na uzalishaji wa mbegu bora za muhogo katika mashamba ya kituo na katika baadhi ya vijiji vya Kanda ya Ziwa na kuzisambaza kwa wakulima. Kituo kwa kushirikiana na Bodi ya Pamba, kitaendelea na uzalishaji wa mbegu mama ya pamba aina ya UK91.

**157. Kituo cha Ilonga (Morogoro)**, kitasambaza mbegu bora za alizeti na soya kwa wakulima vijijini na kuwafundisha wakulima hao teknolojia ya usindikaji wa mbegu za mafuta kwa kutumia mashine za bei nafuu na matumizi ya unga wa soya. Kituo kwa kushirikiana na Bodi ya Pamba kitaendelea kuzalisha pamba aina ya ALAI 90 kwa kutumia wakulima wa mkataba.

**158. Kituo cha Naliendele (Mtwara)**, kitatayarisha tani 24 za mbegu bora za mikorosho na pia kuandaa miche 100,000 kwenye vitalu kwa ajili ya kusambaza kwa wakulima. Aidha, kituo kitatathmini mbegu mpya za karanga ili kuzisambaza kwa wakulima wa Kanda ya Magharibi.

**159. Kituo cha Kibaha (Pwani)**, kitazalisha kwa wingi mbegu mbalimbali za viazi vitamu aina ya *Dakawa*, *Kibaha*, *Ukerewe* na *Simama* zilizopandwa katika hekta 15. Kituo kitazalisha mbegu za muhogo aina ya *Kiroba*, *Kibaha*, *Naliendele 90*, *Mumba* na *Hombolo*. Mbegu hizi zitasambazwa kwa wakulima msimu wa 2003/2004

### Uzalishaji miche kwa njia ya *"tissue culture"*

**160.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004, Wizara itaendeleza teknolojia ya kuzalisha miche kwa njia ya "*tissue culture*" kwenye maabara zilizojengwa katika vituo vya Mikocheni, Mlingano, Tengeru, Uyole na Ukiriguru. Uzalishaji wa miche kwa kutumia teknolojia hii, unawezesha upatikanaji kwa wingi sana, miche yenye ubora sawa na kizazi mama na isiyo na magonjwa. Maabara hizi zitaanza kutoa miche bora ya migomba, muhogo na mananasi katika kipindi hicho. Wakulima wataelimishwa mbinu bora za kilimo cha mazao haya.

### Tathmini ya Mazao ya Viungo na Yasiyo Asili

**161.** Katika mwaka wa 2003/2004, Wizara itashirikiana na wadau mbalimbali, wakiwemo wafanyabishara, katika kuainisha aina za mazao ya viungo na yale yasiyo ya asili kuhusu ubora na sifa zinazotakiwa katika masoko ya nje ya nchi. Inapobidi, aina hizo za mazao hayo zitaingizwa nchini kutoka nje ili zizalishwe kwa wingi na kufikishwa kwa mkulima. Aidha, **Kituo cha KATRIN,** Morogoro kitaendelea kukusanya na kutathmini nasaba *(germplasm)* za mazao hayo kutoka ndani na nje ya nchi na kubaini mazingira yanayofaa na uzalishaji wake.

### Uchunguzi wa Udongo na Kilimo Mseto

**162.** Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na kuzidi kupungua kwa rutuba ya udongo na kuongezeka kwa mmomonyoko wa ardhi katika maeneo mengi nchini, Wizara itaongeza mkazo wa tafiti za kilimo mseto hususan katika maeneo yanayozalisha tumbaku mkoani Tabora kupitia Kituo cha Utafiti cha Tumbi. Aidha, vituo vya Mlingano, Uyole, Seliani na Ilonga vitaendeleza utafiti wa mazao ya jamii ya mikunde yenye kuhifadhi ardhi na kuongeza rutuba katika udongo. Maabara za udongo zilizoko Mlingano, Selian, Uyole na Ukiriguru zitaanza kukarabatiwa chini ya mradi wa PADEP ili ziongeze uwezo wa kuchunguza rutuba ya udongo na kushauri wakulima ipasavyo.

## XXII. HUDUMA ZA UGANI

**163.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004, Wizara itatilia mkazo matumizi ya *mbinu shirikishi jamii* ili kuongeza tija katika sekta ya kilimo na kuimarisha usimamizi wa

huduma za ugani. Kazi kubwa itakuwa kuhakikisha kuwa mipango shirikishi ya vijiji inakuwa msingi wa mipango ya wilaya. Ili kufikia lengo hilo yafuatayo yatafanyika:

- Kuhamasisha Wakuu wa Mikoa na Wilaya na Viongozi Wakuu wa Serikali za Mitaa, kuhusu manufaa na umuhimu wa Mbinu Shirikishi Jamii ili waielewe na kusimamia uenezaji wake katika maeneo yao;
- Kuunda Timu za Wilaya za Wawezeshaji: timu hizo zitatoa mafunzo ya mbinu shirikishi jamii kwa timu za Kata katika wilaya husika. Timu 100 za Wilaya, timu 2,000 za Kata na timu 6,000 za vijiji zitaundwa na kuimarishwa. Timu za kata zikisaidiana na timu za vijiji zitasimamia utekelezaji wa mbinu shirikishi jamii na shamba darasa, kupima maeneo ya mashamba, kuendeleza matumizi ya wanyamakazi na kusimamia utekelezaji wa miradi mingine ya kilimo; na
- Vipindi vya redio vya Mkulima Bora wa Mazao vitaendelea kutolewa mara moja kwa wiki. Aidha, gazeti la Mkulima wa Kisasa litachapishwa na kusambazwa kwa wakulima mara moja kila baada ya miezi miwili.

### Mafunzo kwa Wataalam na Wakulima

**164.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004, kazi zitakazofanyika ni pamoja na:-

- Kukamilisha mitaala mitatu iliyobaki kati ya mitaala minane inayotumiwa kwenye vyuo vya kilimo. Mitaala hiyo inahusu Stashahada ya Kilimo na Lishe, Stashahada ya Hifadhi na Matumizi Bora ya Ardhi na Stashahada ya Kilimo cha Mboga, Matunda na Maua;
- Kufundisha wataalam 750 watakaoshauri wakulima juu ya kanuni bora za kilimo cha mazao ya pamba, kahawa, korosho, chai na tumbaku;
- Kufundisha wakulima 3,000 kanuni bora za kilimo cha biashara. Programu za mafunzo haya zimeandaliwa na kila chuo kulingana na mahitaji ya wakulima wa maeneo yanayohusika;
- Kudhamini mafunzo ya wataalam wa kilimo 250 wenye Astashahada kwa ajili ya mafunzo ya Stashahada katika fani mbalimbali za kilimo na kuandikisha wanafunzi wapya *(pre-service)* 150;
- Kukarabati vyuo na kuvipatia vifaa vya mafunzo kwa vitendo;
- Kuimarisha mafunzo ya wanyamakazi na matumizi ya zana za kilimo vyuoni; na
- Kutoa mafunzo kwa wakulima na wataalam kuhusu kilimo cha umwagiliaji wa zao la mpunga.

## XXIII. KUENDELEZA KILIMO CHA UMWAGILIAJI MAJI MASHAMBANI

**165.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004, lengo la Wizara ya Kilimo na Chakula ni kupanua eneo la uzalishaji kwa kutumia umwagiliaji maji mashambani kwa kuongeza jumla ya hekta 29,397. Ili kufikia lengo hilo, Wizara itaendelea na ujenzi mpya na ukarabati wa skimu za umwagiliaji maji mashambani na kujenga mabwawa ya kuvuna maji yatakayotumika kumwagilia maji mashambani wakati wa kiangazi. Aidha, Wizara itatia mkazo matumizi ya maji ya Ziwa Viktoria kwa ajili ya kumwagilia maji mashambani katika maeneo ya mwambao wa Ziwa hilo.

### Ukarabati wa Skimu za Umwagiliaji Maji Mashambani na Ujenzi wa Mabwawa.

**166.** Skimu 29 za umwagiliaji maji mashambani zilizoainishwa chini ya Mpango Kabambe wa Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani zitakarabatiwa. Skimu hizi zimeonyeshwa katika Kiambatanisho Na. 3. Aidha, Skimu nyingine nne za Nyanzwa (hekta 760) na Irindi (hekta 610) Iringa Vijini, Utengule Usongwe, Mbeya Vijijini (hekta 600) na Naming'ong'o, Mbozi (hekta 1000) ambazo hazikukamilishwa na Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASPS) katika mwaka wa 2002/2003 zitajengwa.

**167.** Mabwawa ya Malolo, Nzega (hekta 100); Igigwa, Sikonge, (hekta 100); Buigiri, Dodoma (hekta 200); Chibumagwa, Manyoni, (hekta 250) yatafufuliwa. Mabwawa ya Mesaga, Serengeti (hekta 170); Nansimo, Bunda (hekta 180) na Chirorwe, Musoma (hekta 80) yaliyosanifiwa na Mradi wa wakulima wa "*Mara Region Farmers Initiative Project'* – (MARAFIP) yatajengwa. Mabwawa mapya ya Mkomazi, Korogwe (hekta 200); Irienyi, Tarime (hekta 250); Tieme – Masagi (hekta 200) na Kironda-datali Iramba (hekta 100) yatasanifiwa na kujengwa.

### Programu Husishi ya Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani

**168.** Katika mwaka wa 2003/2004, Programu hii itaendelea na ujenzi wa majaruba ya mpunga, ujenzi wa miundo mbinu ya umwagiliaji maji mashambani na malambo manne ya kuvuna maji katika skimu 21 zenye hekta 4,669. Skimu hizo zilizo katika wilaya za Babati, Dodoma Vijijini, Manyoni, Nzega, Shinyanga na Kwimba. Aidha, programu itajenga visima 24 na kuwaka pampu za miguu kwa ajili ya kilimo cha bustani na kumwagilia mbegu ya mpunga katika skimu hizo 21.

### Mradi wa Kuendelea Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashamabni Katika Mabonde ya Mito Pangani na Rufiji

**169.** Katika mwaka wa 2003/2004, mradi huu utaendelea kukamilisha ujenzi wa skimu za Kivulini, Mwanga (hekta 410), Longoi, Hai (hekta 300), na Mapogoro, Iringa (hekta 300) na kusimamia uendeshaji wa skimu zilizokamilika. Mradi utakwisha tarehe 31 mwezi wa Desemba 2003.

## XXIV. KUPUNGUZA UPOTEVU WA MAZAO KABLA NA BAADA YA KUVUNA

**170.** Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kuweka mazingira mazuri kuwezesha sekta binafsi kuongeza thamani ya mazao kwa kuanzisha viwanda vya usindikaji. Wizara pia itatoa mafunzo na kusambaza teknolojia bora za utayarishaji, usindikaji na hifadhi ya mazao ya chakula kwa maafisa ugani katika wilaya zote ili kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvuna.

**171.** Wizara itaandaa miongozo ya utayarishaji, usindikaji, ufungashaji na matumizi ya mazao ya chakula hususan muhogo, mtama, viazi vitamu, mboga na matunda ambayo yatatumiwa na maafisa ugani wa Kanda na wilaya kufundishia wakulima. Wizara itandaa na kusambaza mwongozo wa madaraja na viwango vya ubora wa mazao ya chakula.

### Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji

**172.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004, mradi utatekeleza shughuli zake katika Wilaya za Hai, Morogoro Vijijini, Iringa, Singida, Hanang, Arumeru, Masasi na

Nachingwea. Kazi zitakazotekelezwa ni kufanya upembuzi shirikishi katika vijiji vitakavyoshiriki; kutayarisha na kutekeleza miradi ya maendeleo ya kilimo katika vijiji na kutoa mafunzo kwa kamati za miradi. Ili kujenga uwezo wa kuandaa miradi, kufuatilia utekelezaji, udhibiti na uwajibikaji katika matumizi ya fedha; mradi utatoa mafunzo juu ya mbinu shirikishi kwa timu za wawezeshaji za Wilaya na Kata. Mradi utashirikisha sekta binafsi katika kutoa huduma za kitaalamu na kiufundi katika kutekeleza shughuli hizi.

**173.** Mradi utashirikisha wakulima na wafugaji katika kutambua na kuchambua matatizo yao, kubuni mikakati ya kuyatatua kwa kutumia teknolojia sahihi na endelevu katika kuongeza tija katika kilimo na ufugaji. Pia mradi utawezesha wakulima na wafugaji watakaoshiriki kutekeleza mikakati mbalimbali kupitia miradi midogo midogo ya kilimo kwa utaratibu wa "changa nikuchangie". Kwa utaratibu huu, wakulima watachangia asilimia 50 kwa miradi inayohusu matumizi ya pembejeo kwa ajili ya teknolojia mpya na asilimia 20 kwa ajili ya mahitaji mengine yasiyo yapembejeo kwa mfano zana za kilimo. Mradi utachangia asilimia iliyobaki. Aidha, kwa miradi ya vikundi *(Community based projects),* jamii itachangia asilimia 20 ya gharama na mradi utachangia asilimia 80. Utaratibu huu utajenga uwezo wa Halmashauri za Wilaya na taasisi katika kusimamia mipango ya maendeleo ya kilimo; kujenga mazingira mazuri ya uwekezaji; kushirikisha sekta binafsi katika kutoa huduma za kitaaluma, kiufundi na kibiashara.

**174.** Mradi utaanza kufanya ukarabati wa maabara nne za udongo za Mlingano, Uyole, Selian na Ukiriguru ili ziweze kutoa huduma ya upimaji wa udongo kwa mashamba ya wakulima na kushauri matumizi sahihi ya mbolea.

## XXV. UDHIBITI WA VISUMBUFU VYA MIMEA NA MAZAO

**175.** Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti kikamilifu visumbufu vya mimea na mazao, katika mwaka wa 2003/2004, Wizara itaweka mkazo katika masuala yafuatayo:

- Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Kinga ya Mimea *(Plant Protection Act)* ya mwaka wa 1997 na Kanuni zake za mwaka wa 1999, ili kuzuia uingizaji wa visumbufu vya mimea nchini na kuleta ufanisi katika udhibiti wa milipuko ya visumbufu vilivyopo nchini hususan kwelea kwelea, viwavijeshi, panya na nzige.
- Kuendelea kukuza na kueneza teknolojia za udhibiti husishi wa visumbufu vya mimea kwa kutumia mbinu shikishi jamii na shamba darasa.
- Kuimarisha miundombinu ya utabiri wa milipuko ya visumbufu kama viwavijeshi na panya ili kupata na kusambaza taarifa za milipuko mapema
- Kutekeleza Programu ya pamoja ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ya kudhibiti gugumaji hasa kutokana na matatizo ya mto Kagera kuendelea kuingiza gugumaji kwenye Ziwa Viktoria kutoka nchi ya Rwanda.
- Kuweka wilaya za Kibondo, Bukombe na Sengerema chini ya karantini ya ugonjwa wa batobato.
- Kuendesha kampeni za ung'oaji na uchomaji wa miti ya kahawa iliyoathirika na *mnyauko fuzari* na muhogo ulioathiriwa na batobato kwa lengo la kutokomeza magonjwa hayo. Aidha, katika mwaka wa 2003/2004 miche milioni 13 ya aina za muhogo yenye ukinzani dhidi ya batobato itasambazwa katika mikoa ya Kagera, Kigoma, Mwanza na Mara.

**176.** Mheshimiwa Spika, Wizara itaandaa marekebisho ya Sheria ya Hifadhi ya Mimea ya Mwaka 1997 na Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Visumbufu (TPRI) ya Mwaka 1979, ili kuiongezea Taasisi hiyo uwezo wa kiutendaji ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), Shirika la Kibiashara la Kimataifa (WTO) na Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa (FAO).

## XXVI. MATUMIZI YA PEMBEJEO NA ZANA ZA KILIMO

### Mbolea na madawa

**177.** Mheshimiwa Spika, makisio ya mahitaji ya mbolea mwaka wa 2003/2004 yanakadiriwa kuwa tani 185,500 ambapo madawa ya unga yatakuwa tani 21,000 na madawa ya maji yanakadiriwa kuwa lita milioni 4.0. Ili kufanikisha matumizi bora ya pembejeo hizo, Wizara itahamasisha wafanyabiashara kuagiza pembejeo zinazotakiwa, mapema na kuzisambaza. Aidha, Wizara itafuatilia na kutathmini malengo, upatikanaji, usambazaji na matumizi ya pembejeo katika wilaya zote hapa nchini. Wizara itatoa mafunzo juu ya kutunza pembejeo kwa wakala 350 wa pembejeo za kilimo katika mikoa tisa ya Morogoro, Dodoma, Rukwa, Ruvuma, Lindi, Mtwara, Iringa, Arusha na Kilimanjaro.

**178.** Maafisa ugani wakufunzi 120 kutoka wilaya 60 watafundishwa ili wakatoe mafunzo kwa wataalam wengine na wakulima katika wilaya husika kuhusu matumizi bora ya pembejeo, utunzaji na uendeshaji wa biashara ya pembejeo. Wizara itaandaa mkutano utakaoshirikisha wauzaji wa pembejeo na wadau wengine wa pembejeo za kilimo na washauri wa kilimo wa mikoa yote ili kutathmini upatikanaji na matumizi sahihi ya pembejeo. Aidha, Wizara itakamilisha maandalizi ya mapendekezo ya Sheria ya mbolea.

**179.** Mheshimiwa Spika, makisio ya mahitaji ya mbegu zilizothibitishwa katika msimu wa 2003/2004 ni tani 30,000. Upatikanaji wa mbegu unategemewa kuwa jumla ya tani 12,310, ambao utatokana na uzalishaji katika mashamba ya makampuni binafsi nchini (tani 1,628), wakulima wadogo (tani 700), uagizaji kutoka nje (tani 8,482) na uzalishaji katika mashamba ya Serikali tani 1,500. Kazi nyingine zitakazofanyika msimu wa 2003/2004 ni:

- Kudhibiti ubora wa mbegu nchini, chini ya usimamizi wa wakala wa Ukaguzi na Udhibiti wa Mbegu (TOSCA). Ili kuimarisha shughuli za udhibiti, wataalam wa kilimo 20 wakiwemo maafisa ugani wa wilaya na wakaguzi wa mazao mipakani watapewa mafunzo ya jinsi ya kukagua mbegu.
- Kukamilisha maandalizi ya kuanzisha Wakala wa Mbegu wa Serikali.
- Kuzalisha mbegu za daraja la kuazimiwa kwa kutumia wakulima wadogo chini ya Mradi wa ASPS katika mikoa ya Dodoma, Morogoro, Iringa, Lindi, Mtwara na Pwani ambapo jumla ya vijiji 220 vitahusishwa.
- Kutoa mafunzo ya uzalishaji mbegu kwa vikundi 18 vya wakulima wanaoshiriki katika kuzalisha mbegu za daraja la kuazimiwa katika wilaya sita za Bunda, Musoma (Mara), Misungwi (Mwanza), Shinyanga, Dodoma na Mwanga (Kilimanjaro).
- Kuanzisha Ofisi ya Msajili wa Hakimiliki za aina mpya za mbegu na mimea mipya (*Plant Breeders Right*).

**180.** Katika mwaka wa 2003/2004, Serikali imetenga shilingi milioni 500 kufidia gharama za usafirishaji wa pembejeo muhimu hasa mbolea kwa ajili ya mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

## Zana za Kilimo

**181.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004, Wizara ya Kilimo na Chakula itatoa mafunzo ya matumizi ya wanyamakazi katika wilaya 76 za mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Mara, Tabora, Singida, Dodoma, Morogoro, Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Mtwara, Ruvuma, Kigoma, Mbeya, Rukwa, Iringa, Manyara na Pwani. Vituo 40 vya wanyamakazi katika wilaya hizo vitakarabatiwa na kupatiwa zana ili viweze kutoa mafunzo na kufanya maonyesho kwa wakulima juu ya matumizi bora ya teknolojia ya wanyamakazi katika kilimo. Kila kituo kitaanzisha shamba la mfano la ekari 5 kwa ajili ya kutoa mafunzo.

**182.** Mafunzo ya matumizi bora ya zana zinazokokotwa na wanyamakazi yatatolewa kwa maafisa ugani 912 na wakulima wakufunzi 1,000. Wakulima wakufunzi hao watapewa zana ili watoe mafunzo kwa wakulima wenzao vijijini kwa kushirikiana na maafisa ugani.

**183.** Mheshimiwa Spika, ili kuendeleza kilimo cha matrekta, Wizara itatoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wakulima kupitia mfuko wa pembejeo ili waweze kununua matrekta mapya na vipuri vya kukarabati matrekta mabovu. Jumla ya matrekta 243 katika mikoa ya Dodoma, Arusha, Mbeya, Shinyanga, Mwanza, Iringa na Kilimanjaro yatakarabatiwa kwa kutumia utaratibu huo. Halmashauri za Wilaya kwa kutumia waatalam wake, zitahusika katika tathmini ya awali ya matrekta na kutoa mapendekezo ya wakulima watakaopewa mikopo. Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri, zitadhibiti ubora wa kazi ya ukarabati. Aidha, kituo kimoja cha kukodisha matrekta kitakachoendeshwa na sekta binafsi, kitaanzishwa mkoani Kilimanjaro ili kitoe huduma kwa wakulima.

**184.** Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kutoa mafunzo juu ya matumizi ya matrekta madogo ya mkono kwa mafundi sanifu 40 kutoka Morogoro (8), Arusha (2), Kigoma (6), Rukwa (6), Singida (5), Tabora (4), Mara (4), Kilimanjaro (3) na Mbeya (2). Mafunzo kuhusu matumizi ya mashine ndogo za kubangua korosho yatatolewa kwa mafundi sanifu 30 kutoka Ruvuma (9), Tanga (9), Mtwara (6) na Pwani (6). Mafundi sanifu hao watatoa mafunzo kwa wakulima vijijini. Wizara pia itaendelea kutoa ushauri kwa wakulima na taasisi mbalimbali juu ya matumizi ya zana za aina mbalimbali za wanyamakazi, matrekta na usindikaji wa mazao.

# XXVII. MATUMIZI BORA YA ARDHI

**185.** Mheshimiwa Spika, uzalishaji katika kilimo hutegemea sana ubora na rutuba ya udongo. Utafiti uliofanywa na Wizara mwaka wa 1995, ulibaini kwamba wastani wa tani 5 hadi 15 za udongo kwa hekta hupotea kila mwaka kutokana na mmomonyoko wa udongo unaosababishwa na maji na upepo kutokana na matumizi mabaya ya ardhi.

**186.** Kasi ya uharibifu na upotevu wa ardhi na udongo wenye rutuba imefikia kiwango cha kutisha. Ili kuunusuru udongo na ardhi, hatua za haraka zinapaswa kuchukuliwa. Kwa bahati nzuri, mbinu za kukabiliana na mmomonyoko wa udongo zinafahamika na wananchi wengi. Mbinu hizo ni pamoja na kulima kilimo cha matuta na makinga maji. Mbinu nyingine ni kupanda miti au mimea mingine ya kuzuia kasi ya maji na upepo.

**187.** Katika mwaka wa 2003/2004, Wizara itaboresha na kueneza teknolojia zinazotumika kuhifadhi udongo na maji mashambani ambazo tayari zimeonyesha matokeo mazuri. Ili kufikia malengo haya, Wizara itatoa mafunzo kwa maafisa ugani 48 na wakulima wakufunzi 160 watakaowafundisha wakulima wengine 1,600 kutoka Wilaya za Iringa, Morogoro, Mbinga, Magu, Tarime, Dodoma Vijijini, Korogwe, Handeni, Rombo, Kigoma na Kasulu.

**188.** Kazi nyingine zitakazofanyika ni kuhimiza kilimo cha matuta ya kuzuia mmomonyoko wa udongo, kuendeleza kilimo mseto, na kuvuna maji ya mvua katika wilaya za Arumeru, Mbulu, Babati, Monduli, Rombo, Hai, Korogwe, Lushoto, Muheza, Kwimba, Magu, Sengerema, Geita, Ukerewe na Shinyanga.

**189.** Mheshimiwa Spika, ili kupunguza migogoro ya ardhi katika jamii na kuvutia uwekezaji katika kilimo, Wizara itashirikiana na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Halmashauri za Wilaya na wadau wengine kutenga maeneo ya ardhi ya kilimo na matumizi mengine.

## XXVIII. MFUKO WA PEMBEJEO

**190.** Mheshimiwa Spika, mwaka wa 2003/2004, Mfuko wa Pembejeo utaendelea kutoa mikopo kwa ajili ya uagizaji na usambazaji wa pembejeo na zana za kilimo kwa kupitia mabenki. Aidha, utaratibu umeandaliwa wa kutoa mikopo kwa ajili ya kununulia matrekta mapya pamoja na kukarabati ya zamani. Mikopo itatolewa kwa masharti ya ukopeshaji ya benki na wakopaji watapaswa kurejesha mikopo kwa kufuata utaratibu uliokubaliwa kati yao na benki.

**191.** Mheshimiwa Spika, ili kufikisha huduma za Mfuko wa Pembejeo kwa Wakulima na wafugaji Mfuko huo umekubaliana na mabenki kutoa huduma za mikopo mikoani kama ifuatavyo:-

- Benki ya Exim – mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Tanga, Mtwara, Lindi, Arusha, Manyara, Dodoma, Singida, Mbeya, Ruvuma, Morogoro na Rukwa;
- Benki ya Ushirika Kilimanjaro – Mkoa wa Kilimanjaro;
- Benki ya Wananchi ya Mufindi - Wilaya ya Mufindi;
- Benki ya Kimataifa ya Malaysia (T) Ltd. Mikoa ya Mwanza, Mara, Shinyanga, Tabora na Kigoma; na
- Shirikisho la Vyama vya Ushirika vya Kuweka na Kukopa Tanzania (1992) Ltd - SACCOS/SACCAS itahuduma wanachama wake nchi nzima.

**192.** Wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa mawakala na wasambazaji wa pembejeo ili kuboresha huduma hii. Ukusanyaji madeni ya nyuma utaendelea ikiwa ni pamoja na uuzaji wa dhamana za wadaiwa baada ya kupata hukumu za kesi zao ambazo ziko mahakamani. Hadi sasa kuna kesi 78 za wadaiwa ambazo bado zinaendelea kwenye mahakama mbalimbali nchini.

## XXIX. USALAMA NA HIFADHI YA CHAKULA

### Usalama wa Chakula

**193.** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo na Chakula inalo jukumu la kuhakikisha kuwa Taifa linakuwa na upatikanaji na usalama wa chakula wakati wote. Katika mwaka wa 2003/2004, Wizara itaendelea na kazi ya kufuatilia takwimu na taarifa za mvua na hali ya mazao mashambani kwa kufanya tathmini mbali mbali za hali ya chakula nchini. Aidha, mfumo wa kuhifadhi takwimu na taarifa za usalama wa chakula katika ngazi ya Taifa utaendelezwa na maandalizi ya kuanzisha mfumo huo katika ngazi ya wilaya yatafanyika. Pamoja na kazi hii, Wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa Watakwimu Kilimo wa mikoa na wilaya na wakusanya taarifa na takwimu za mvua na mazao mashambani kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa takwimu hizo na kujenga uwezo katika ngazi ya wilaya na mikoa.

**194.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara itaendesha mafunzo kwa maafisa ugani wa wilaya zote na wale wa kanda kwa kusudi la kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvuna. Wizara itaandaa miongozo ya utayarishaji na matumizi ya mazao ya chakula hususan, muhogo, mtama, mboga na matunda, kwa ajili ya wawezeshaji wa kanda na wilaya zote ili kuboresha lishe na kupunguza utapiamlo katika jamii. Aidha, mwongozo wa mafunzo ya kusindika, kufungasha, hifadhi ya muhogo na viazi vitamu, utasambazwa kwa maafisa ugani wa kata zote katika mikoa inayolima mazao hayo.

## XXX. HIFADHI YA CHAKULA

**195.** Mheshimiwa Spika, mwaka wa 2003/2004, Hifadhi ya Chakula ya Taifa itanunua jumla ya tani 20,799 za mahindi kutoka hapa nchini zenye thamani ya shilingi bilioni 3.026. Chakula hicho kitahifadhiwa katika Kanda saba za Hifadhi ya Chakula ya Taifa, na endapo upungufu utatokea, kitapelekwa na kuuzwa kwenye maeneo yenye upungufu wa chakula.

## XXXI. KUREKEBISHA NA KUHUISHA SHERIA

**196.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004, Wizara itaendelea kufanya maandalizi ya marekebisho ya Sheria, taratibu na Kanuni za Bodi za Korosho, Chai na Pareto. Marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Korosho ya Mwaka wa 1984 na Muswada wa Sheria ya Bodi ya Mazao Mchanganyiko yatawasilishwa Bungeni. Maandalizi ya marekebisho ya Sheria na Kanuni za Bodi za Chai na Pareto yatafanyika. Wizara pia itawasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya kusimamia uvunaji wa nasaba za mimea kwa ajili ya Chakula na Kilimo *(Plant Genetic Resources Exploitation and Control).*

## XXXII. FEDHA ZA STABEX

**197.** Chini ya utaratibu wa Stabex (1992-1994), Jumuia ya Nchi za Ulaya imetoa jumla ya Shilingi bilioni 37 zitakazotumika katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwezi wa Julai, 2003. Fedha hizo zitagharamia utafiti wa zao la kahawa (shilingi bilioni 9), ujenzi na ukarabati wa barabara za mikoa (shilingi bilioni 10), na kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo, hususan kutekeleza miradi chini ya Mipango ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo ya Wilaya *(District Agricultural Development Plans-DADPs)* (shilingi bilioni 18).

**198.** Mheshimiwa Spika, ningependa kuwafahamisha kwamba kuna masharti maalum ya matumizi ya fedha za kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo chini ya utaratibu wa Stabex. Upatikanaji wa fedha hizo utategemea kibali kutoka Jumuia ya Nchi za Ulaya baada ya kuwasilisha miradi na mipango ya kuendeleza kilimo, mifugo, na ushirika inayokidhi vigezo vilivyowekwa. Ili fedha hizo ziweze kutolewa, Halmashauri za wilaya zinatakiwa kuandaa mipango ya kuendeleza sekta ya kilimo kwa kuzingatia Mwongozo wa Kuandaa Mipango hiyo na kiwasilisha Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Katika mwaka wa 2003/2004, jumla ya shilingi bilioni 3 zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya.

## XXXIII. UBINAFSISHAJI WA MASHAMBA YA KILIMO

**199.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004, Wizara itafuatilia utekelezaji wa mikataba ya mauzo ili kuhakikisha kuwa malengo ya ubinafsishaji wa mali ya umma yanatekelezwa. Maeneo yatakayofuatiliwa ni mashamba ya mkonge, mpunga, ngano na viwanda vya chai, tumbaku, kahawa na sukari. Pia Wizara itafuatilia vinu vya Shirika la Usagishaji la Taifa (NMC) vilivyobinafsishwa.

**200.** Katika mwaka wa 2003/2004, Mali ambazo zimepangwa kubinafsishwa ni pamoja na Kiwanda cha Chai cha Lupembe, Shamba la Chai la Mlangali, viwanda 12 vya korosho, mashamba ya mkonge, Kampuni ya Kahawa ya TANICA na jineri ya Bodi ya Pamba iliyoko Manawa. Mashamba ya mahindi ya Mbozi na Namtumbo, mashamba ya ngano ya Hanang na mashamba ya West Kilimanjaro yatahamishiwa na kujumuishwa kwenye Benki ya Ardhi inayosimamiwa na Kituo cha Uwekezaji cha Taifa (TIC).

## XXXIV. MAENDELEO YA WATUMISHI

**201.** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo na Chakula itaendelea kurekebisha vyeo vya watumishi wa Wizara ili vilingane na vile vya wenzao wenye sifa zinazofanana walioko kwenye Wizara nyingine za Serikali. Hatua zitakazochukuliwa ni :

- Kuwatambua watumishi wote ambao hawajafikia vyeo wanavyostahili hata baada ya kupandishwa vyeo viwili viwili.
- Kuomba kibali Ofisi ya Rais, Idara Kuu ya Utumishi ili wapandishwe vyeo kufikia madaraja wanayostahili.
- Kutayarisha mapendekezo na kuyatuma Tume ya Utumishi Serikalini ili wahusika wapandishwe vyeo vilivyoidhinishwa na Idara Kuu ya Utumishi.

**202.** Wizara itaendelea kuhamasisha na kuelimisha watumishi jinsi ya kuhuisha jinsia katika sekta na kujikinga na janga la UKIMWI.

## XXXV. HITIMISHO

**203.** Mheshimiwa Spika, Sekta ya Kilimo ni muhimu sana katika uchumi wa Taifa na ukuaji wa sekta hii utachangia kukua kwa sekta nyingine za uchumi. Ili sekta hii ikue kwa kiwango cha asilimia 10 hadi 11, kiwango ambacho kitaleta maendeleo na kuondoa umaskini na kuhakikisha upatikanaji na usalama wa chakula ushirikiano wa wadau wote wa sekta ya kilimo hususan Halmashauri za Wilaya ni muhimu. Aidha, **kilimo hakina budi kuendeshwa kwa mipango iliyoandaliwa kwa makini na inayoweka utaratibu mzuri wa usimamizi.** Halmashauri za Wilaya hazina budi kuweka utaratibu wa kutumia *Mbinu Shirikishi Jamii* katika kuandaa na kusimamia Mipango ya Kilimo.

**204.** Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie hotuba yangu kwa kurejea matarajio ya hali ya chakula katika mwaka wa 2003/2004. Kama nilivyosema awali, hali ya chakula haitazamiwi kuwa ya kuridhisha kutokana na athari za ukame katika baadhi ya maeneo ya nchi msimu uliopita. Hivyo, kutakuwepo na upungufu wa chakula katika maeneo yaliyoathirika. Ili kukabiliana na hali hiyo, ninatoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge, Wakuu wa Mikoa na Wilaya na watendaji wote katika ngazi zote kuendelea kuhamasisha, kuhimiza, kuelekeza na kusimamia kikamilifu utekelezaji wa maagizo ya Rais ya tarehe 31 Machi, 2003. Mambo muhimu ya kuzingatia ili kutekeleza maagizo hayo, ni kuhakikisha kuwa wakulima wanalima mazao yanayostahimili ukame hususan muhogo na yale yanayokomaa haraka na kusimamia utekelezaji wake. Wakulima na wananchi kwa ujumla waelekezwe kutumia kwa uangalifu chakula kilichopo na kujiwekea akiba. Aidha, wafugaji wauze sehemu ya mifugo yao wakati bei zikiwa bado ni nzuri na mifugo ikiwa na afya nzuri ili wapate fedha za kujinunulia chakula.

## XXXVI. SHUKRANI

**205.** Mheshimiwa Spika, natoa shukrani za dhati kwa nchi na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa ambayo yanaendelea kuisaidia Wizara ya Kilimo na Chakula katika juhudi za kuleta mapinduzi katika sekta ya kilimo. Nchi hizo ni Denmark, China, Canada, Finland, India, Ireland, Israel, Italia, Japan, Korea ya Kusini, Marekani, Misri, Ubelgiji, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Uswisi na Sweden. Napenda pia kuyashukuru Mashirika na Taasisi za Kimataifa kama ifuatavyo: Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, UNDP, FAO, JICA, DFID, EU, UNICEF, WFP, IFAD, CIMMYT, ICRAF, ICRISAT, ASARECA, USAID, GTZ, IITA na Sasakawa Global 2000. Bado tunahitaji misaada na ushirikiano wao ili kuendeleza kilimo nchini.

**206.** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za pekee kwa wakulima wa nchi hii kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuendeleza kilimo. Aidha, napenda kutambua mchango mkubwa unaotolewa na wanawake na wazee waishio vijijini katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara na shughuli nyingine za uzalishaji katika sekta ya kilimo. Mwisho, natoa shukrani kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kazi nzuri ya kuchapa hotuba hii.

## XXXVII. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA 2003/2004

**207.** Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo haya, ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 54,146,806,100.00. Kati ya hizo, shilingi 22,628,841,900 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 31,517,964,200.00 ni kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo, shilingi 6,436,433,200.00 ambayo ni sawa na asilimia 20.4 ni fedha za hapa na shilingi 25,081,531,000. 00 ambayo ni sawa na asilimia 79.6 ni fedha za nje.

**208. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.**

*Kiambatanisho Na. 1*

## Tathmini ya Awali ya Chakula kwa mwaka 2003/04 - Utabiri uliotolewa tarehe 16/5/2003

(Kutokana na Tathmini Awali ya Mavuno (Preliminary forecast) ya 2002/03 inayozingatia Taarifa za Hali ya Mvua na Mazao Mashambani kufikia 16/5/2003)

| | Matarajio ya Mazao ya Nafaka | | | | Matarajio ya Mazao Yasiyo Nafaka | | | | Jumla ya Matarajio ya Mavuno Yote | | | | | Upu - ngufu |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mkoa | Mavuno | Mahitaji | Upungufu -/ Ziada | Kiwango cha Kujitosheleza (Nafaka) | Mavuno | Mahitaji | Upungufu -/ Ziada | Kiwango cha Kujitosheleza (Yasiyo Nafaka) | Mavuno | Mahitaji | Upungufu -/ Ziada | Kiwango cha Kujitosheleza (Chakula) | Mkoa | (*) |
| Arusha+Manyara | 267,054 | 386,269 | (119,216) | **69** | 162,253 | 234,546 | (72,294) | **69** | 429,306 | 620,816 | (191509) | **69** | **Arusha+Manyara** | * |
| Pwani | 61,343 | 137,296 | (75,953) | **45** | 101,049 | 86,021 | 15,028 | **117** | 162,392 | 223,317 | (60925) | **73** | **Pwani** | * |
| Dar es Salaam | 7,439 | 377,817 | (370,379) | **2** | 28,493 | 247,311 | (218,818) | **12** | 35,932 | 625,128 | (589197) | **6** | **Dar es Salaam** | * |
| Dodoma | 163,751 | 268,240 | (104,489) | **61** | 145,711 | 164,169 | (18,458) | **89** | 309,462 | 432,409 | (122947) | **72** | **Dodoma** | * |
| Iringa | 373,009 | 259,848 | 113,161 | **144** | 142,662 | 143,074 | (412) | **100** | 515,671 | 402,922 | 112749 | **128** | **Iringa** | |
| Kagera | 119,766 | 282,707 | (162,942) | **42** | 456,664 | 198,459 | 258,205 | **230** | 576,430 | 481,166 | 95264 | **120** | **Kagera** | |
| Kigoma | 152,503 | 222,385 | (69,883) | **69** | 330,217 | 167,244 | 162,972 | **197** | 482,719 | 389,630 | 93090 | **124** | **Kigoma** | |
| Kilimanjaro | 189,630 | 203,288 | (13,658) | **93** | 146,468 | 132,312 | 14,156 | **111** | 336,098 | 335,599 | 499 | **100** | **Kilimanjaro** | |
| Lindi | 59,328 | 162,972 | (103,644) | **36** | 121,844 | 75,619 | 46,225 | **161** | 181,172 | 238,591 | (57419) | **76** | **Lindi** | * |
| Mara | 149,517 | 211,437 | (61,920) | **71** | 184,523 | 132,568 | 51,955 | **139** | 334,040 | 344,005 | (9966) | **97** | **Mara** | * |
| Mbeya | 377,705 | 305,581 | 72,124 | **124** | 208,108 | 200,268 | 7,841 | **104** | 585,813 | 505,849 | 79965 | **116** | **Mbeya** | |
| Morogoro | 204,951 | 260,420 | (55,469) | **79** | 159,313 | 170,671 | (11,358) | **93** | 364,264 | 431,091 | (66827) | **84** | **Morogoro** | * |
| Mtwara | 83,845 | 165,166 | (81,322) | **51** | 237,647 | 108,244 | 129,404 | **220** | 321,492 | 273,410 | 48082 | **118** | **Mtwara** | |
| Mwanza | 289,074 | 438,584 | (149,511) | **66** | 372,378 | 287,433 | 84,945 | **130** | 661,452 | 726,018 | (64566) | **91** | **Mwanza** | * |
| Rukwa | 271,491 | 171,028 | 100,462 | **159** | 88,544 | 112,086 | (23,542) | **79** | 360,034 | 283,114 | 76921 | **127** | **Rukwa** | |
| Ruvuma | 182,149 | 165,119 | 17,031 | **110** | 109,787 | 108,212 | 1,575 | **101** | 291,937 | 273,331 | 18606 | **107** | **Ruvuma** | |
| Shinyanga | 370,924 | 418,735 | (47,812) | **89** | 212,790 | 274,425 | (61,635) | **78** | 583,714 | 693,160 | (109446) | **84** | **Shinyanga** | * |
| Singida | 105,575 | 160,821 | (55,246) | **66** | 103,185 | 105,396 | (2,212) | **98** | 208,760 | 266,217 | (57458) | **78** | **Singida** | * |
| Tabora | 243,305 | 257,335 | (14,030) | **95** | 168,864 | 168,649 | 215 | **100** | 412,169 | 425,984 | (13815) | **97** | **Tabora** | * |
| Tanga | 165,116 | 240,615 | (75,499) | **69** | 234,582 | 157,691 | 76,891 | **149** | 399,698 | 398,306 | 1392 | **100** | **Tanga** | |
| **JUMLA TANZANIA** | **3,837,473** | **5,095,666** | **(1,258,193)** | 75 | **3,715,081** | **3,274,397** | **440,684** | 113 | **7,552,554** | **8,370,063** | (817509) | 90 | **JUMLA TANZANIA** | * |

***Kiambatanisho Na. 2***

*Utekelezaji wa Skimu Chini ya Mpango Husishi wa Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani, 2003/2004*

| WILAYA/ SKIMU | ENEO (HEKTARI) | IDADI YA WALENGWA | HALI YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| **Babati** | | | |
| Mawemairo/Matufa | 362 | 446 | Ujenzi unaendelea |
| Gichameda | 154 | 247 | Ujenzi utaanza, July 2003 |
| Qash | 206 | 164 | Ujenzi utaanza, July 2003 |
| **Dodoma** | | | |
| Uhelela | 134 | 180 | Ujenzi utaanza, July 2003 |
| Mpwayungu | 140 | 323 | Ujenzi utaanza, July 2003 |
| Mtitaa | 106 | 215 | Ujenzi utaanza, July 2003 |
| **Manyoni** | | | |
| Mtiwe | 153 | 318 | Ujenzi umekamilika |
| Msemembo | 200 | 410 | Ujenzi unaendelea |
| Udimaa | 416 | 340 | Ujenzi utaanza, July 2003 |
| **Nzega** | | | |
| Chamipulu | 250 | 284 | Ujenzi utaanza, July 2003 |
| Ifumba | 298 | 402 | Ujenzi umekamilika |
| Lakuyi | 93 | 163 | Ujenzi utaanza, Septemba 2003 |
| Mwasala | 225 | 400 | Ujenzi utaanza, July 2003 |
| Sigiri | 153 | 270 | Ujenzi utaanza, July 2003 |
| **Shinyanga** | | | |
| Masengwa | 337 | 257 | Ujenzi utaanza, July 2003 |
| Itilima | 224 | 204 | Ujenzi utaanza, July 2003 |
| Nyida | 289 | 209 | Ujenzi utaanza, Augusti 2003 |
| Butini | 415 | 410 | Ujenzi umekamilika, March 2003 |
| **Kwimba** | | | |
| Kimiza | 153 | 493 | Ujenzi utaanza, July 2003 |
| Luhala | 160 | 344 | Ujenzi utaanza, July 2003 |
| Shilanona | 201 | 233 | Ujenzi utaanza, July 2003 |
| **JUMLA** | **4,669** | **6,312** | |

*Kiambatanisho Na. 3*

***Skimu 29 Zitakazokarabatiwa, 2003/2004***

| S/NA | JINA LA SKIMU | MKOA | WILAYA | ENEO (HA) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Engaruka | Arusha | Monduli | 215 |
| 2 | Kisese | Dodoma | Kondoa | 120 |
| 3 | Mbuyuni | Iringa | Iringa | 600 |
| 4 | Kalenga-Ongoing | Iringa | Iringa | 240 |
| 5 | Igoma | Iringa | Mufindi | 120 |
| 6 | Nkenge | Kagera | Bukoba | 500 |
| 7 | Ruhwiti | Kigoma | Kibondo | 300 |
| 8 | Muhwazi-expansion | Kigoma | Kibondo | 500 |
| 9 | Msambara | Kigoma | Kasulu | 600 |
| 10 | Musa Mwinjanga | Kilimanjaro | Hai | 676 |
| 11 | Siha | Kilimanjaro | Hai | 120 |
| 12 | Kikafu chini-expansion | Kilimanjaro | Hai | 641 |
| 13 | Chikoko | Lindi | Rwanga | 200 |
| 14 | Suguti | Mara | Musoma | 2000 |
| 15 | Butiama | Mara | Musoma | 300 |
| 16 | Ochuna | Mara | Tarime | 300 |
| 17 | Kasyabone | Mbeya | Rungwe | 600 |
| 18 | Mshewe | Mbeya | Mbeya | 300 |
| 19 | Mbebe | Mbeya | Illeje | 556 |
| 20 | Mvumi | Morogoro | Kilosa | 260 |
| 21 | Mahurunga | Mtwara | Mtwara | 1000 |
| 22 | Katunguru | Mwanza | Sengerema | 1000 |
| 23 | Nkonkwa | Kigoma | Kigoma (v) | 440 |
| 24 | Kalemela | Mwanza | Magu | 20 |
| 25 | Katuka | Rukwa | Sumbawanga | 250 |
| 26 | Lufwi | Rukwa | Nkasi | 2000 |
| 27 | Liyuni | Ruvuma | Namtumbo | 400 |
| 28 | Magoma | Tanga | Tanga | 350 |
| 29 | Kwemazandu | Tanga | Korogwe | 120 |
| | | | **TOTAL** | **14,728** |